**ACT:** Tutaondoa viongozi wote watakaojihusisha na rushwa

UKURASA 2

**UCHAGUZI TLS**
Karatasi za kura zaongezwa, Lissu adai hakuna mizengwe

UKURASA 3



**BITEKO** ang'aka mifugo kuingizwa katika mashamba ya wakulima

UKURASA 4




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Agosti 3, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581757

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# 'Kuna shida ufujaji mapato bandarini'

UKURASA 7

## Waandishi wa IPP Media wang'ara tuzo umahiri wa uandishi wa habari

UKURASA 4



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (wa tatu kushoto), akiwa katika picha ya pamoja na waandishi wa habari wa IPP Media walioshinda Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari za Tulia Trust 2024, baada ya kukabidhiwa tuzo zao katika hafla iliyofanyika jijini Mbeya usiku wa kuamkia jana. Kutoka kushoto ni Nerbart Msokwa wa Nipashe (Mshindi wa Tuzo ya Mpigapicha Bora), Christina Mwakangale wa Nipashe (Mshindi wa Habari za Watoto), Halfani Chusi wa Nipashe (Mshindi wa Habari za Uchunguzi), Rebecca Kinyunyu wa ITV (Mshindi wa Habari za Uchunguzi) na Kenneth Ngelesi wa EATV (Mshindi wa Habari za Uchunguzi). **Habari zaidi Uk. 4. PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Sengerema, mkoani Mwanza, Sajini Selina Manda akimwonya na kumpa elimu ya usalama barabarani mwendesha pikipiki, maarufu bodaboda, baada ya kumkamata kutokana na kukiuka sheria katika eneo la Mapinda, mjini Sengerema juzi. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Rais Samia aahidi neema wakulima

**AONYA** wananchi kuchagua viongozi wabovu Uchaguzi Serikali za Mitaa...*ukurasa 2*

**MICHEZO** **FADLU AITA MASHABIKI KUIONA SIMBA MPYA** UK 24

MAONI, KATUNI UK.6

# ACT: Tutawaondoa viongozi watakaojihusisha na rushwa

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI wakuu wa ACT Wazalendo wameguswa na malalamiko ya wananchi kuhusu vitendo vya ubabe na kutowajibika kwa baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa na vijiji katika kutatua matatizo ya wananchi.

Wamewataka wananchi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapigakura ili kuchagua viongozi watakaowajibika kwao na kuondoa viongozi waliodai wamewekwa madarakani kwa mabavu.

Kauli hizo zimeelezwa viongozi wa ACT Wazalendo wakiwa katika mwendelezo wa ziara ya chama awamu ya kwanza katika mikoa 22, majimbo 125 Tanzania Bara. Ziara hiyo imo katika majimbo ya Longido (Arusha), Tandahimba (Mtwara), Ukerewe (Mwanza) na Sumbawanga (Rukwa).

Zitto Kabwe, Kiongozi wa Chama mstaafu, akiwa mjini Sumbawanga juzi, aliwaeleza wananchi wa Rukwa kuwa njia mwafaka hivi sasa kuondoa viongozi hao ni kushiriki ipasavyo katika uchaguzi wa mwaka huu kwa kuchagua viongozi wenye maarifa na uchungu na umasikini.

"Nchi yetu ni nchi ya kidemokrasia, tunapaswa kuilinda demokrasia na kuitumia kama gurudumu la maendeleo, tusikubali kususa wala kukata tamaa, tujiandikishe katika Daftari la Wapigakura, tujiandikishe kuwa wanachama wa ACT Wazalendo na tuchague wagombea madhubuti wa chama chetu, ni lazima tuchukue hatua hii muhimu na lazima tuanze sasa," alisema.

Akiwa Longido, Kiongozi wa Chama, Dorothy Semu alieleza vilio vya wananchi kutosikilizwa kwa kero zao na kutowajibika kwa viongozi wa serikali za mitaa.

"Nimepita vijijini, nimekutana na matatizo makubwa. Kupata utambulisho kwa kiongozi wa kijiji ni kwa malipo, kuzuka kwa faini za ovyo na uonevu. Viongozi wanafanya uamuzi mkubwa bila vikao vya uamuzi, wanauza maeneo (viwanja) kwa ubabe na vitisho kwa kushirikiana na viongozi wa serikali kuu, jambo hili halikubaliki hata kidogo, ni lazima wananchi tuchukue hatua ya kuwaondoa," alisema.

Kiongozi wa Chama aliwaeleza wananchi kuwa katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wana nafasi ya kuzuia mateso hayo kuendelea tena kwa miaka mitano mingine kwa kuwa njia pekee ya kuleta mabadiliko ipo mikononi mwao kwa kuchagua mabadiliko.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Isihaka Mchinjita, akiwa Tandahimba alisema: "Ukiona kobe juu ya mti si nguvu zake, kuna aliyempandisha. Viongozi wa Serikali za Mitaa na Vijiji wote ni matokeo ya kilichojiri katika uchaguzi wa mwaka 2019, hivyo hawawezi kuhudumia wananchi."

Alisema ACT Wazalendo itaendelea kupigania kuundwa na kutekeleza kazi zake kisheria za Tume Huru ya Uchaguzi, huku ikijiandaa kuipeleka serikali mahakamani kupinga Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kusimamiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Akiwa katika Jimbo la Ukerewe, Katibu Mkuu, Ado Shaibu alifanya mkutano wa hadhara na kuwaambia wananchi wa Ukerewe kuwa ACT Wazalendo imejizatiti kukutoa viongozi jasiri na madhubuti watakaosimama na wananchi kwa kuondoa kabisa vitendo vya ruswa.

"Tutawaondoa viongozi wote watakaojihusisha na vitendo vya rushwa, vitisho na uonevu. Tutaweka utaratibu wa tathmini ya utendaji kwa viongozi kupitia mikutano ya wananchi vijijini.

"Tutaweka hatua kali za kupambana na rushwa ili kila shilingi iwe inatumika kwa manufaa ya watu. Pia kuchukua hatua za kisheria na kiutawala, kwa haraka, dhidi ya vitendo vya rushwa," alisema.

Viongozi hao wamendelea na ziara katika mikoa yote Tanzania. Jana walitarajiwa kuwa katika majimbo ya Nyamagana (Mwanza), Nanyamba (Mtwara), Nkasi (Rukwa) na Arumeru Magharibi (Arusha).



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akimjulia hali mgonjwa aliyelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Gairo, baada ya kuizindua hospitali hiyo, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Morogoro jana. **PICHA: IKULU**

# Samia aahidi neema wakulima

**Na Idda Mushi,** GAIRO

RAIS Samia Suluhu Hassan amehimiza wananchi kuendelea kuzalisha zaidi mazao ya chakula na biashara na kuahidi serikali kuendelea kuwatafutia masoko ya uhakika.

Rais Samia alisema hayo jana akiwa wilayani Gairo, mkoani Morogoro ikiwa ni siku ya kwanza ya ziara yake ya siku sita mkoani humu, akimwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kuweka mikakati itakayowezesha mbaazi kupata soko na bei nzuri kama ilivyo kwa korosho kwa mikoa ya kusini.

Akizungumza na wananchi baada ya kuzindua Hospitali ya Wilaya ya Kilosa na baadaye Daraja la Berega linalounganisha wananchi na Hospitali ya Berega, Rais Samia alisema anajua zao la mbaazi halina bei nzuri sokoni ndio maana anataka jitihada za makusudi kupata soko na bei ya uhakika.

Alisema amefika Morogoro pamoja na mambo mengine kusikiliza shida za wananchi na kuzifanyia kazi, kuona matokeo ya fedha za maendeleo zinazotolewa, kuzindua, kukagua na kuweka jiwe la msingi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kuangalia urejeshwaji miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko kutokana na mvua ya El- Nino.

Rais Samia aliyeridhishwa na matumizi ya fedha katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Gairo, aliwataka wananchi mkoani Morogoro kujipanga kwa ajili ya Uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa na kuzingatia kuchagua viongozi bora ili kufikiwa na maendeleo.

Kuhusu changamoto ya maji wilayani Gairo, Mkuu wa Nchi alisema iko mbioni kutatauliwa baada ya serikali kutoa Sh. bilioni 34 kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji; mikataba imeshatiwa saini.

Alisema kuwa Wilaya ya Gairo inakwenda kuondokana na changamoto ya kukatika ovyo kwa umeme baada ya serikali kujenga kituo cha kupokea, kupooza na kusambaza umeme katika wilaya jirani ya Kongwa, mkoani Dodoma.

"Gairo mna bahati sana kama alivyosema Mbunge wenu (Ahmed Shabiby), changamoto zote zilizokuwa zimeahidiwa zimetatuliwa na hizi zilizotajwa hapa pia zote tutakwenda kuzifanyia kazi.

"Niko na mawaziri wangu na wakati mbunge wenu anazitaja niliona kila mmoja ana kalamu, anaziandika vizuri," alisema Rais Samia aliyeongozana na mawaziri 10 na wasaidizi wao wizarani.

Awali Mbunge wa Gairo, Shabiby, alipongeza serikali chini ya Rais Samia kwa kutekeleza ahadi nyingi hasa zilizoahidiwa na Rais ndani ya kipindi cha miaka mitatu na nusu aliyokaa madarakani ikiwamo ujenzi wa Kituo cha Afya Nongwe, Magereza na Mahakama.

Mafanikio mengine aliyataja ni utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa madaraja mawili moja lenye urefu wa mita 80 na lingine urefu wa mita 100 ambayo yana uwezo wa kupita magari mawili yanayounganisha na barabara ya lami ya kwenda Kilindi sambamba na mfereji mkubwa wa kuzuia mafuriko.

Alisema kuwa hivi sasa barabara zote za Gairo zinapitika hadi milimani na kuna mawasiliano ya simu na miundombinu ya barabara.

Alisema serikali ilitoa zaidi ya Sh. bilioni 18 kwa ajili ya miradi ya elimu na afya na kuomba serikali kuongeza fedha zaidi kwa ajili ya dawa na gari la wagonjwa wa dharura kutokana na eneo hilo kuhudumia wananchi wa Kiteto na Kilindi na limekuwa likipokea majeruhi wa ajali mara kwa mara katika barabara kuu ya Morogoro-Dodoma.

"Tunaomba serikali itupatie pia ruzuku ya mbegu za alizeti kwa wananchi na itujengee soko la kisasa na stendi (kituo cha mabasi) ya wilaya," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ya Rais Samia, mambo makubwa ya kizalendo yamefanyika na kugusa maisha ya Watanzania wa hali ya chini ikiwamo katika sekta za elimu na afya.

Alisema kwa Wilaya ya Gairo, zahanatii mpya 32 zilijengwa pamoja na hospitali ya wilaya iliyogharimu zaidi ya Sh. bilioni tisa ambayo haikuwapo awali.

"Kwa kipindi hiki tu cha miaka mitatu karibu na nusu chini ya uongozi wako Mheshimiwa Rais, zaidi ya wananchi 12,335 wamepata huduma katika hospitali hii, lakini kuna wagonjwa wa dharura zaidi ya 700.

"Fedha zinazotolewa na serikali zimesogeza huduma karibu kabisa na wananchi wakiwamo wananchi wanyonge, kazi hizi zote zinatosha kukunadi," alisema Waziri Mchengerwa.



Mtaro maalum kwa maji ya mvua uliopo eneo la Uzuri Kilimani Manzese, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, ukiwa na majitaka jana, ambayo yanatiririshwa kutoka katika vyoo, kitendo ambacho kinahatarisha afya za watu. **PICHA: SABATO KASIKA**

UCHAGUZI TLS

# Karatasi za kura zaongezwa, Lissu adai hakuna mizengwe

**Na Romana Mallya**

UPIGAJI kura uchaguzi wa urais Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) jana ulilazimika kusogezwa mbele kwa muda na baadaye kuendelea baada ya karatasi za kupigia kura kupelea.

Wanachama wa TLS walikuwa wakipiga kura kadri wanavyofika eneo husika na mchakato huo ulitarajiwa kufungwa saa 6:00 mchana, lakini kabla ya muda huo, karatasi za kupigia kura zilikwisha na mchakato huo kusimama kusubiri nyingine.

Baada ya hali hiyo kutokea, Kamati ya Uchaguzi ilitangaza kuongeza saa moja ili kukamilisha muda uliopangwa.

Uchaguzi huo ulianza saa 12:30 asubuhi katika viwanja vya Kituo cha Mikutano cha Jakaya, jijini Dodoma, ambako vituo kadhaa vya kupigia kura viliwekwa na mawakili walijitokeza kutimiza haki yao ya msingi huku askari polisi wakisimamia usalama.

Katika nafasi ya urais wagombea sita waliochuana ni Boniface Mwabukusi, Ibrahim Bendera, Emmanuel Muga, Revocatus Kuuli, Paul Kaunda na Sweetbert Nkuba. Wagombea wengine wanawania nafasi nyingine ndani ya TLS.

Baada ya karatasi kwisha, mmoja wa wagombea urais, Wakili Mwabukusi alisema wamekubaliana ziongezwe angalau karatasi 200 ili wote waliofika huko kupiga kura watimize wajibu wao wa msingi.

"Muda uliopangwa uchaguzi kumalizika ni saa sita mchana, lakini waliokwenda kuchapisha karatasi wakirejea wataongeza dakika 60 (saa moja) za kuendelea kupiga kura," alisema mgombea huyo.

Tundu Lissu ambaye ni miongoni mwa waliopiga kura jana, alisema mchakato huo umekwenda vizuri kama ilivyokuwa miaka yote.

"Sisi chama cha mawikili tunaendesha uchaguzi huru na za haki hakuna mizengwe. Chama cha Mawakili ni taasisi ambayo katika kila nchi, kinasimamia masuala muhimu ya umma na utawala wa sheria," alisema Lissu, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Alisema kusipokuwa na utawala wa sheria, kunakuwa na utekaji nyara, viongozi kufukuza watu kwa maelfu katika maeneo yao, kuuawa, kufunguliwa kesi za uongo na kuonewa.

Lissu alisema wajibu wa Chama cha Mawakili pamoja na kuwakilisha wateja wao mahakamani na masuala mengine ya kisheria, wajibu wake ni kusimamia utawala wa sheria na "kuhakikisha nchi inaendeshwa sawasawa".

"Hivyo, unahitaji uongozi wa chama unaotambua hayo na ambao utakuwa tayari kuyasemea. Watu wanashangaa Chama cha Mawakili wa Kenya wanakwenda mahakamani na kusema Rais huna mamlaka ya kuamuru jeshi kuingia barabarani kukulinda, huo ndio wajibu wa mawakili kutetea katiba na utawala wa sheria," alisema.

Hivyo, Lissu alisema Chama cha Mawakili na mawakili wenyewe wanapojitambua hufanya wajibu wao.

Alipoulizwa kuhusu uanaharakati ndani ya TLS kunakosababisha mgawanyiko, Lissu alisema wasipokuwa na TLS inayozungumza, maana yake wanakuwa na chama kilicholala.

Alisema nchi inaharibika, mawakili wakinyamaza; wakizungumza kwa sauti moja nchi inasikiliza.

"Leo (jana) watu wote wanasubiri moshi mweupe (kupatikana kiongozi mpya) Dodoma, mawakili watachangua nini? Watachagua nani? Kwa sababu taifa linatambua kwamba mawakili wakisema si sawasawa na mtu yeyote akisema, haya majina wanaharakati tangu lini ni neno baya.

"Kuwa na chama cha wanasheria wanaojitambua ni jambo jema kwa nchi. Wajibu wa wanasheria si kuinyamazia serikali, ni kuisema inapokosea," alisema.

Lissu alisema uchaguzi huo ni tukio muhimu kwa sababu linaamua kuwa na wanasheria wanaowasemea au wanaoangalia maslahi yao.

Watakaochaguliwa na kutangazwa wanatarajia kuapishwa leo katika Mkutano Mkuu unaoendelea jijini Dodoma.

# TRC yaomba radhi treni ya SGR kuchelewa kisa hitilafu

**Na Romana Mallya**

UONGOZI wa Shirika la Reli (TRC) umeomba radhi wateja wake kutokana na kuchelewa kuwasili kwa muda uliotarajiwa, treni yake ya abiria.

Imeelezwa kuwa hitilafu ya kiufundi ya treni ya abiria ya kawaida ilitokea Mtaa wa Mshikamano, Kata ya Kihonda, mkoani Morogoro na kusababisha wasafiri waliokuwa wakitokea Dodoma kwenda Dar es Salaam kuchelewa kuwasili jijini humo juzi usiku.

Tatizo hilo lilitokea baada ya Jumanne wiki hii hitilafu ya umeme kutokea kati ya Stesheni ya Kilosa na Kidete, mkoani Morogoro na kusababisha treni ya shirika hilo kusimama kwa muda wa saa mbili na kuzua mjadala mtandaoni.

Mjadala huo uliibuka baada ya TRC kueleza kwamba, taarifa za awali zinaonesha hitilafu za aina hiyo husababishwa na wanyama kama ngedere au ndege aina ya bundi.

Juzi baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuzindua rasmi usafiri huo wa treni za umeme katika reli ya kisasa (SGR), ilipotimu saa 2:15 usiku, abiria waliokuwa wanasafiri kwenda Dar es Salaam walikutakana na kadhia nyingine ya hitilafu ya kiufundi huku shirika hilo likiomba radhi kwa mara nyingine.

"Hitilafu za kiufundi zilitokea majira ya saa 4:33 usiku na kushughulikiwa kwa muda wa takribani saa moja na kusababisha treni hiyo ya abiria kutoka Dodoma kuchelewa kuwasili Dar es Salaam kwa wakati uliopangwa," ilisema taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano TRC, Jamila Mbarouk.

Kutokana na hali hiyo, Jamila alisema shirika linatoa taarifa kuwa treni ya abiria iliyobeba viongozi na wananchi wengine waliotoka Dodoma saa moja usiku baada ya kushiriki sherehe za uzinduzi wa SGR waliwasili Dar es Salaam kwa muda uliopangwa bila hitilafu yoyote.

Alisema shirika hilo linazingatia usalama wa abiria kabla na wakati wa safari ili kuepuka madhara kwa watumiaji wa huduma za usafiri wa reli na kuomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza.

Baada ya hitilafu ya awali kutokea, shirika hilo lilisema "Taarifa za awali zinaonesha kuwa hitilafu za aina hiyo husababishwa na wanyama (ngedere) au ndege (bundi) wanapogusa nyaya za umeme zilizotandazwa juu ya reli.

"Hitilafu ilisababisha umeme kukatika katika kituo cha kupooza umeme namba saba (Godegode) ambayo kitaalam hujulikana kama (Instanteneous Overcurrent Protection Trip) majira ya saa 4:20 usiku," TRC ilieleza katika taarifa yake.

Shirika hilo lilifafanua zaidi kuwa mafundi wake walitatua changamoto hiyo na kurejesha umeme saa 6:30 usiku na treni hiyo kuendelea na safari kwenda Dodoma na kuwasili saa 7:57 usiku.



Magari yakiwa kwenye foleni kubwa katika eneo la Kimara Mwisho Dar es Salaam jana, inayosababishwa na shughuli za upanuzi unaoendelea wa barabara ya Morogoro. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waandishi wa IPP Media wang'ara tuzo umahiri wa uandishi wa habari

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAANDISHI wa habari sita wa IPP Media wameibuka washindi katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari za Tulia Trust Journalism Awards (TJA) 2024.

Washindi hao ni: Nebart Msokwa-Nipashe (Mshindi wa Tuzo ya Mpigapicha Bora); Christina Mwakangale-Nipashe (Mshindi wa Habari za Watoto); Halfani Chusi-Nipashe (Mshindi wa Habari za Uchunguzi) na Rececca Kinyunyu-ITV (Mshindi wa Habari za Uchunguzi).

Wengine ni Kenneth Ngelesi-EATV (Mshindi wa Habari za Uchunguzi) na Asha Athuman-Nipashe (Mshindi wa Habari za Gesi na Uchimbaji Madini). Tuzo hizo zimetolewa usiku wa kuamkia jana, jijini Mbeya.

Akizungumza baada ya kutolewa kwa tuzo hizo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema tuzo hizo hutolewa kila mwaka kwa lengo la kutambua mchango wa waandishi wa habari katika jamii.

Alisema waandishi wa habari ni miongoni mwa makundi muhimu ambayo yanatambuliwa kwa tuzo hizo za Taasisi ya Tulia Trust iliyojikita katika kutoa msaada na kuinua jamii hususan wazee, vijana, wanawake na watoto katika shughuli mbalimbali.

"Tuzo hizi tutaendelea kuziboresha kila mwaka kwa kuwa tunatambua mchango mkubwa wa waandishi wa habari nchini.

"Ni imani yangu wigo wa ushiriki utazidi kuongezeka tukipata washiriki kutoka kila mkoa nchini. Mwaka huu tumepata baadhi ya washindi kutoka Dar es Salaam," alisema Dk. Tulia.

Kazi za uandishi wa habari zinazoshindanishwa katika tuzo hizo ni zilizohusu Mkoa wa Mbeya.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alisema pamoja na kazi nzuri wanayofanya waandishi wa habari, wasisahau kujiimarisha kiuchumi kuhakikisha wanatumia uandishi wao kuinua kipato binafsi.

"Mnapokuwa katika majukumu yenu, hakikisheni mnatumia vyema nafasi yenu kujiinua kiuchumi. Msijisahau kwa ajili ya maisha yenu ya baadaye, hasa kupitia tuzo hizi," alisema Malisa.

Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera alisema ubunifu alioufanya na Dk. Tulia ni wa kuigwa kutokana na kuthamini taaluma ya habari ambayo imeajiri watu wengi.

Tuzo hizo zilikuwa na vipengele 16, zikiwavutia washiriki 157, lakini ni 32 tu ambao kazi zao zilipitishwa na jopo la majaji kuingia hatua ya fainali.

Washindi wa kwanza kwa kila kipengele walipatiwa fedha taslimu Sh. milioni moja kila mmoja; washindi wa pili Sh. 500,000 kila mmoja na nafasi ya tatu Sh. 300,000 kila mmoja huku mshindi wa jumla akipata Sh. milioni moja.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wakiongozwa na Spika wa Bunge ambaye pia ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia, ambaye pia ni Mbunge wa Mbeya Mjini na Mkurugenzi wa Tulia Trust.

# Biteko ang'aka mifugo kuingizwa katika mashamba ya wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri Mkuu ameagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi ishirikiane na wakuu wa mikoa kudhibiti wafugaji kuingiza mifugo katika maeneo ya wakulima ili kuzuia migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara na kuhatarisha amani.

Watendaji hao wa serikali pia wameagizwa kushirikiana kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi na kuhakikisha inafuatwa, msisitizo ukiwa kufundisha wakulima na wafugaji kufanya shughuli hizo kisasa ili kuongeza tija.

Dk. Dotto Biteko alitoa maagizo hayo jana alipofungua Maonesho ya Wakulima, maarufu Nanenane, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo yanafanyika katika Uwanja wa John Mwakangale, jijini Mbeya.

Alisema matumizi bora ya ardhi yatasaidia kuondoa migogoro kati ya binadamu na wanyama wakali ambao wamekuwa wakibugudhi mifugo na binadamu hasa katika maeneo ya pembezoni mwa hifadhi za taifa.

"Shirikianeni kuwafundisha wafugaji kuhusu utunzaji malisho na kuchimba malambo katika vitalu vya kuchungia ili kuongeza tija ya uzalishaji na kupunguza migogoro hiyo," alisema Dk. Biteko.

Aliwataka wakulima, wafugaji na wavuvi kufuata maelekezo ya wataalamu kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu na kemikali ili kuepuka madhara ya kemikali hizo kwa binadamu, viumbehai vingine na mazingira.

Naibu Waziri Mkuu Biteko pia aliwataka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kushirikiana kulinda maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya utafiti wa kilimo ili kuongeza uzalishaji mbegu na kupunguza uingizaji mbegu kutoka nje ya nchi.

"Maofisa ardhi msiende kupima maeneo hayo kwa ajili ya makazi, tutasababisha nchi yetu kuwa mteja wa mbegu na viuatilifu kutoka kwenye mataifa ambayo yamelinda maeneo yake ya utafiti, yalindeni kwa wivu mkubwa" aliagiza Dk. Biteko.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde alisema serikali imewekeza nguvu kubwa katika kuboresha kilimo nchini kutokana na sekta hiyo kuajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania na kuwa chanzo kikuu cha malighafi za viwandani.

Alisema bajeti ya kilimo imeongezwa kutoka Sh. bilioni 294 mwaka wa fedha 2022/23 mpaka Sh. trilioni 1.2 mwaka huu na hivyo kufanya sekta hiyo kuwa miongoni mwa sekta zenye bajeti kubwa.

Alisema kuwa kutokana na ongezeko hilo la bajeti, hata kiwango cha ukuaji wa sekta ya kilimo kimeongezeka kutoka asilimia 2.7 mpaka asilimia 4.2 huku ongezeko la utoshelevu wa chakula likifikia asilimia 130.

Vilevile, Slinde alisema wanaendelea na uboreshaji viwanja vya maonesho hayo katika kanda mbalimbali ili kuongeza tija na kwamba wameanzia Uwanja wa Dodoma na watafuata viwanja vingine.

"Tulielekezwa na Rais kuboresha viwanja hivi na niwathibitishie kwamba baada ya maonesho haya tunaanza uboreshaji wa Uwanja huu wa John Mwakangale, mkandarasi ameshapatikana, anasubiri tumalize maonesho ili aendelee na kazi," alisema Silinde.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alisema kitendo cha serikali kuweka ruzuku kwenye mbolea na pembejeo zingine za kilimo, kimesababisha ongezeko la matumizi ya pembejeo hizo kwa wakulima na hivyo kuongeza uzalishaji.

Alisema mbali na kuweka ruzuku hiyo, pia imeweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa hizo, hali ambayo imesaidia kuongezeka kwa upatikanaji wake nchini.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema mikoa ya nyanda hizo imekuwa inaongoza kwa uzalishaji chakula nchini na hivyo kutumika kama kapu la chakula la taifa.

# MATUKIO KATIKA PICHA




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akivuta pazia kuzindua Hospitali ya Wilaya ya Gairo, baada ya kuanza ziara yake ya kikazi, mkoani Morogoro jana. Wengine ni Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa (kushoto) na Mkuu wa Mkoa huo, Adam Malima. **PICHA: IKULU**



Watoto wakiangalia wanyama katika moja ya mabanda ya ufugaji kwenye Maonesho ya 31 ya Kilimo ya Nane Nane yanayoendelea katika viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Ofisa Misitu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Rogasian Lukoa, akizungumza wakati wa kikao cha kamati ya kitaifa ya usimamizi wa Mradi wa Urejeshwaji endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai Tanzania (SLR), kilichofanyika mjini Iringa, hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Takataka zikiwa zimetelekezwa bila ya kuzolewa katika makutano ya barabara ya kuingia kwenye Soko la Buguruni na Mtaa wa Madenge, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji akijitambulisha kwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kulia), alipofanya ziara yake Ofisini kwa Makamu wa Kwanza Migombani, Zanzibar jana. **PICHA: OMR**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuzo ziwe chachu kwa wachezaji wazawa

**USIKU** wa juzi tumeshuhudia hafla ya kufana ya utoaji wa tuzo kwa wachezaji, makocha na timu zilizofanya vizuri kwenye msimu uliopita wa 2023/2024.

Tuzo hizo ni ishara ya kukamilisha msimu uliopita na kuanza mchakato wa kuanza msimu mpya wa 2024/2025 ambao unatarajiwa kuanza Agosti 16 baada ya michezo ya Ngao ya Jamii itakayochezwa wiki ijayo.

Kwa mara nyingine tena tumeshuhudia tuzo za msimu uliopita wachezaji wageni wakitawala zaidi kuliko wachezaji wazawa ambao kiujumla ndio wapo wengi kwenye ligi kuu.

Hata hivyo tuzo hizo zimeangalia zaidi uwezo wa wachezaji na kile walichokifanya kwa timu zao kwa msimu uliopita.

Pamoja na ukweli kuwa tuzo nyingi zilizotolewa zimeenda kwa wachezaji wa kigeni, bado kuna kitu cha kujifunza kwa wachezaji wa nyumbani.

Tuzo zilizotolewa hazikuwa kwa bahati mbaya kwa wachezaji wa kigeni, bali zimetokana na kile walichokionesha kwenye ligi Kuu msimu uliopita ambao Yanga waliibuka mabingwa.

Kwa mfano, nyota wa Yanga, Stephane Aziz Ki ameibuka kuwa kinara wa tuzo kwa kubeba tuzo nne peke yake. Kwa tuliofuatilia michezo ya Ligi Kuu msimu uliopita wala hatushangai kuona mchezaji huyo raia wa Burkina Fasso akitwaa tuzo hizo zote.

Aziz Ki msimu uliopita aliibeba timu yake mabegani kwa kuchangia ushindi katika michezo mingi aliyocheza na kupelekea kuutetea ubingwa wao kwa msimu wa tatu mfululizo.

Kile kilichofanywa na Aziz Ki kinaweza kikafanywa na wachezaji wetu wazawa kama wataendelea kujituma na kujiwekea malengo katika uchezaji wao.

Tuzo zilizochukuliwa na wachezaji wa kigeni zimeendelea kutoa somo kwa wachezaji wetu wa ndani juu ya kujituma na uwajibikaji kwenye klabu zao.

Wachezaji wetu lazima wakumbushwe kuwa mpira ni kazi kama kazi nyingine lakini utofauti wake ni muda mfupi wa kufanya kazi hiyo, mpira ni kazi ya muda mfupi.

Itapendeza kwa misimu ijayo tukishuhudia wachezaji wazawa wakitawala tuzo na kuwafunika wachezaji wageni, hayo yanawezekana kama watajituma na kuonyesha uwezo wao wote uwanjani.

Na hili pia lipo kwa makocha wetu wazawa, miaka mingi tunaona tuzo ya kocha bora wa msimu ikienda kwa makocha wa kigeni kutokana na kile wanachokifanya kwenye timu zao.

Makocha wetu wazawa nao wana nafasi ya kuchukua tuzo hizi kwa kuhakikisha wanatoa ujuzi wao kuzisaidia timu zao kufanya vizuri na ikiwezekana kutwaa ubingwa siku moja.


Nipashe tunawapongeza wale wote waliotwaa tuzo za msimu uliopita, na tunaamini tuzo zimetolewa kwa kuzingatia uwezo na kile walichokifanya kwenye timu zao.

Lakini bado tunasisitiza tuzo hizi ziwaamshe wachezaji wazawa kujituma na kufanya vizuri uwanjani ilikuzisaidia timu zao kufikia malengo yao, tunaamini nafasi ya kuchukua tuzo hizi bado wanazo.

Tuzo zimepita, Shirikisho la soka Tanzania (TFF) wamefunga shughuli za msimu uliopita, sasa ni wazi mlango kuelekea msimu mpya umefunguliwa, kazi ipo kwa wachezaji na makocha kuwapa burudani mashabiki na wapenzi wa soka.

==

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mastaa wajifunze kuongea na media,yasiwakute ya Makabila

**MOJA** kati ya vitu vilivyozua mjadala kwenye mitandao ya kijamii wiki hii ni baadhi ya wanachama na mashabiki wa Simba kumkataa msanii maarufu wa singeli, Dulla Makabila afanye onesho leo katika tamasha la kilele cha siku yao, maarufu kama Simba Day.

Mitandao wa kijamii 'ilichafuka' mara baada kuhabarishwa kuwa Makabila atakuwa mmoja wa watakaotumbuiza Simba Day.

Sababu kubwa ni kwamba alishawahi kuwaponda Simba siku za nyuma, huku wakiposti video fupi iliyoonekana anawananga Wekundu wa Msimbazi.

"Mimi siipendi Simba, tena siipendi kutoka moyoni, hata ikicheza na wagonjwa, mimi nitashangilia hao wagonjwa,"ilisikika video hiyo ikimuonesha Makabila akiongea siku za nyuma.

Mashabiki hao walifukua makaburi wakidai alisema maneno hayo alipokuwa kwenye onesho la kilele cha Wiki ya Mwananchi.

Ikawa sasa kama kuna kampeni fulani hivi, kiasi kwamba mpaka Makabila mwenyewe akaamua kuomba msamaha kwenye mtandao wake wa instagram.

"Kwanza naomba nichukue nafasi hii kuwaomba radhi mashabiki wote wa Simba kwa kauli mbaya nilizowahi kutoa kipindi cha nyuma zilizosababisha kuwakwaza.

Pili naomba kesho niwape zawadi yenu ya wimbo tutakaoutumia kwenye siku ya Simba Day," ilikuwa ni sehemu ya maneno aliyoyaandika.

Wengine walimuelewa na wengine bado waliendelea kusimamia msimamo wao, na baada ya muda, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally akaandika kuwa watawapa kile ambacho mashabiki wao wanakihitaji na kama kuna msanii hawamtaki, basi itakuwa hivyo.

"Hili ni tamasha la kuwapa burudani mashabiki wa Simba, ni tamasha lao hili, sasa kama mashabiki hawamtaki msanii kwa nini tumuweke? Hatupo kuwaudhi mashabiki wetu na klabu haijamtangaza Dulla kama atatumbuiza siku hiyo, hadi sasa Simba tumemtangaza msanii mmoja tu atakayetumbuiza ambaye ni Ali Kiba," aliandika.

Kwa nini haya yote yametokea?, yamesababishwa na Makabila mwenyewe. Vyovyote vile, kama atatumbuiza leo au la, lakini anapaswa ajifunze kuchunga mdomo wake kwani, ukishakuwa maarufu, iwe msanii, mwanamuziki au mchezaji wewe ni kama mfanyabiashara na nembo, hutakiwi kuegemea upande mmoja au kuongea maneno ya kuudhi kwa kile kitu ambacho hukipendi.

Tunajua kuna wachezaji ambao ni mashabiki wa Yanga wameshachezea Simba, na wa Simba pia wamechezea Yanga tena kwa weledi na baadaye sana ndiyo watu wamejua mapenzi yao moyoni yapo wapi. Ukishakuwa ni 'brandi', hutakiwi kuwa na mihemko ya ushabiki, chuki, au chochote ambacho kitakuweka mtegoni baadaye.

Hata zamani, wanamuziki kama Muhidini Gurumo, Hassan Bitchuka ni wanachama Simba, lakini bendi zao zilikuwa zinapiga Jangwani pale Yanga ikitwaa ubingwa, na TX Moshi William alikuwa Yanga wa kutupwa, lakini Msondo Ngoma ilikuwa ikipiga dansi maalum Simba inapokuwa bingwa na wala hawakuwahi kuziponda, licha ya kwamba watu wanajua itikadi zao, lakini kinachotazamwa hapo ni weledi tu.

Ndiyo maana utaona mtu kama Ali Kiba, anayedaiwa shabiki wa Yanga, ndiye mtumbuizaji mkuu kwenye tamasha la leo na Diamond Platnumz, ambaye inasemwa kuwa ni Simba damu, atakuwa akiwatumbuiza mashabiki wa Yanga.

Hawa hawajawahi kutamka kibaya chochote cha kukwaza kuhusu timu hizo, hivyo wamechukuliwa bila kuangalia itikadi zao, kinachotakiwa hapo ni muziki tu. Na hili ni funzo kwa wasanii, wanamuziki na wachezaji wote nchini. Wao ni kama wafanyabiashara, hivyo ni lazima walinde nembo zao kwa kujifunza kuongea kistaarabu na kuheshimu watu na taasisi nyingine mbele ya vyombo vya habari licha ya kwamba kuna ushindani.

Nadhani hili ndilo tatizo kubwa la wanamuziki, wasanii na wanamichezo wa Kitanzania, kutojua waongee nini mbele ya kamera na vipaza sauti kutokana na kutofundishwa tangu mwanzo.

Wenzetu huko nje, anapokuwa msanii mkubwa, au wakati akiwa kwenye akademi, moja ya mambo wanayofundishwa ni jinsi gani ya kuongea mbele ya wanahabari, kudhibiti mihemko, kula, kuvaa, kuishi, na vingine vinavyofanana na hivyo ili kulinda 'brandi' yake na kuongeza wigo wa biashara na kutotaka kuwapoteza wateja au wapenzi wake. Lililojitokeza liwe funzo kwa wote.

HABARI KITAIFA

# Samia kuweka jiwe la msingi upanuzi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero

**Na Mwandishi Wetu**

UPANUZI wa Kiwanda cha Sukari cha Kilombero, Mkoani Morogoro unatarajiwa kuongeza uwezo wake wa kuzalisha sukari kutoka tani 126,000 kwa mwaka hadi kufikia tani 271,000 ifikapo mwakani.

Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Derick Stanley, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uwekaji jiwe la msingi kiwandani huko utakaofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kesho.

Alisema upanuzi huo ni mkakati wa kuunga mkono juhudi za serikali kuhakikisha nchi inakuwa na sukari ya kutosha.

"Kiwanda cha Sukari Kilombero kipo mbioni kukamilisha upanuzi wa kiwanda chake cha K4, unaogharimu Sh. bilioni 744 na unatarajia kukamilika mwezi Juni 2025.

"Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza uwezo wa kampuni hiyo katika kuzalisha sukari kutoka tani 126,000 kwa mwaka hadi kufikia tani 271,000 ifikapo mwaka 2025," alisema.

Stanley alisema kiwanda hicho cha K4 kilianza kujengwa miaka miwili iliyopita, akitamba kuwa ni cha kisasa na kinachoongoza kwa ukubwa Afrika Mashariki.

"Kukamilika kwa kiwanda hiki kutapunguza changamoto za uhaba wa sukari nchini, hivyo kusaidia serikali kutoagiza bidhaa hiyo nje ya nchi," alisema.

Stanley alisema mradi huo utaleta mapinduzi makubwa kiuchumi, ikiambatana na Dira ya Taifa kwamba, ifikapo mwakani nchi iwe na utoshelevu wa sukari ya matumizi ya majumbani.

Stanley alisema kupitia kiwanda hicho cha K4, kutakuwa na ongezeko la mapato kwa wakulima wa Bonde la Kilombero kutoka Sh. bilioni 75 hadi kufikia takribani Sh. bilioni 165 kwa mwaka. Hiyo itakuwa sambamba na ongezeko la idadi ya wakulima kutoka 8,000 hadi kufikia watu 16,000.

Meneja wa Masuala ya Biashara wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Willa Haonga, aliwataka kinamama kuchangamkia fursa ya mradi huo kwa kuwa utafiti unaonesha wanaume ndiyo wanaongoza kwa biashara ya kilimo cha miwa.




Mkurugenzi wa Mahusiano na Mawasiliano Kampuni ya Sukari Kilombero, Derick Stanley (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro juzi, kuhusu uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa upanuzi wa kiwanda cha Kilombero K4 kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya sukari nchini, unaotarajiwa kufanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kesho. Wengine ni Meneja Mawasiliano na Mahusiano kwa Wadau, Victor Byemelwa (kushoto) na Meneja wa Biashara, Willa Haonga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Kuna mianya ya ufujaji mapato bandarini'

**Na Adela Madyane,** KIGOMA

UTARATIBU wa ukusanyaji mapato katika Bandari ya Kibirizi iliyoko Manispaa ya Kigoma Ujiji, mkoani hapa, umelalamikiwa kuwa chanzo kikuu cha mianya ya rushwa ambayo huleta hasara kwa serikali.

Baadhi ya wajumbe walioshiriki kikao cha Baraza la Biashara la Mkoa kilichofanyika jana katika Ukumbi wa Lake Tanganyika, mjini hapa, walisema makusanyo mengi ya tozo hayaingii serikalini kwa kuwa yanatozwa kiholela bila mpangilio maalum.

Walisema katika mazingira hayo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Mamlaka ya Mapato (TRA), Forodha na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) hukusanya mapato kwa njia tofauti na kusababisha upotevu wa mapato.

Alhaji Mabie, mfanyabiashara kutoka kampuni ya usafirishaji wa mizigo na abiria Aifola, alisema abiria wanaosafiri kwa kutumia meli za mizigo zilizoidhinishwa ili kupunguza changamoto za usafiri kuelekea Congo, hutozwa kati ya Dola 25 hadi Dola 30 kama malipo ya tiketi ilhali hawapewi tiketi za kielektroniki.

"Bado wahusika wanatumia teknolojia ya zamani. Abiria hawakati tiketi katika mfumo maalum, kinachofanyika wanaandikwa majina na mtu wa meli, wanatozwa Dola 25 au Dola 30 kisha anazichukua mtu anayekata tiketi na hakuna sehemu yoyote inayoonesha asilimia za tozo zinazoingia serikalini. Serikali iongeze usimamizi, izuie mianya ya rushwa," alisema Mabie. Alisema fedha nyingi zinapotea, akitolea mfano wa fedha za udongo kiasi cha Dola tano zinazolipwa na wageni kutoka Congo pindi waingiapo nchini ambazo alidai hazina risiti wala maelezo yoyote, jambo linalofanya serikali ipoteze mapato mengi kupitia lango la uchumi na biashara la bandari.

Mabie alisema wafanyakazi wa serikali wanapaswa kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake kutimiza wajibu wao kikamilifu kwa kufuata miongozo, kanuni na sheria za nchi ili serikali inufaike na tozo.

"Tozo nyingine zote ndogo zinazokusanywa na taasisi mbalimbali kama za mionzi na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ziwekwe katika mfumo mmoja wa malipo ili kuondoa urasimu ulioko," alishauri.

Mwenyekiti wa kikao hicho, Thobias Andengenye, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, alisema wafanyabiashara wako tayari kulipia tozo hizo.

"Iwe Dola moja au Dola tano zinazokusanywa, zinapaswa kuingia serikalini. Ninawashukuru wafanyabiashara wa Kigoma kwa kuwa hawajawahi kuwa na tatizo la kulipa tozo ila shida ni kuwa fedha zinakusanywa kienyeji na badala ya kusaidia serikali zinamsaidia mtu mmoja. Tunataka fedha hizi zisaidie kupunguza changamoto kwa wananchi wetu," alisema Andengenye.

Baraza hilo pia limepiga marufuku abiria kuingia ndani ya meli akiwa hana tiketi ya safari na hayupo katika orodha ya wanaosafiri, ili kuimarisha salama katika vyombo hivyo na kudhibiti ufujaji mapato.

Pia limeagiza taasisi zinazohusika na usafirishaji TRA, uhamiaji, TPA na TASAC kuanzisha mfumo wa pamoja wa ukusanyaji mapato kwa taasisi zote zinazohusika bandarini ili kurahisisha ufuatiliaji na udhibiti wa mapato.

Mwajuma Ally, mchumi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa (Sekta ya Uchumi, Viwanda, Biashara na Uwekezaji), alisema ili kutatua kero hiyo tayari kamati imeundwa kutafuta ufumbuzi namna ya kuziweka tozo hizo pamoja ili kumwondolea usumbufu mfanyabiashara.

Alisema kuwa hiyo si mara ya kwanza kwa wafanyabiashara kulalamikia tozo hizo na walishawasilisha hoja hizo katika taasisi husika, ingawa utekelezaji wake haukuzaa matunda.

Alisema hiyo ndiyo sababu wamekubaliana kuwa na mfumo wa pamoja ambao wanaamini utakuwa suluhu ya upotevu huo wa makusanyo hayo.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Walimu 1,000 watembelea Mikumi kwa SGR

## -RC Chalamila apongeza mikakati ya NMB

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila ameipongeza Benki ya NMB kwa jitihada zake za kuendelea kusaidia ustawi wa walimu nchini.

Chalamila alitoa pongezi hizo jijini Dar es Salaam jana. wakati wa hafla ya kuwaaga walimu 1,000 walioanza ziara ya siku mbili iliyopewa jina la SGR-Mikumi.

Ziara hiyo imefadhiliwa na Benki ya NMB, taasisi hiyo ya fedha ikitoa Sh. milioni 22. Kati yake, Sh. milioni 12 ni gharama za kuchapa fulana na Sh. milioni 10 kwa ajili ya mambo mengine.

"Benki ya NMB imekuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono juhudi mbalimbali za maendeleo zinazoanzishwa na serikali. Ninatumia fursa hii pia kuipongeza benki hii kwa kuunga mkono ziara hii ya walimu," Chalamila alisema.

Aliongeza, "Walimu ni kundi la kwanza kufanya ziara ya mradi wa reli ya SGR baada ya kuzinduliwa rasmi na Rais Samia Suluhu Hassan Alhamisi wiki hii.

"Ninaamini kuwa ziara hii si tu itaongeza maarifa na uzoefu kwa walimu, bali pia itakuwa chachu ya kampeni ya Tanzania The Royal Tour."

Chalamila alibainisha kuwa katika mkakati wa muda mrefu wa kutangaza mradi wa reli ya SGR, ofisi yake imeandaa na kuratibu ziara nyingine tarehe 30 Agosti mwaka huu ambayo itakutanisha vikundi maalumu.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Toba Nguvila wakati wa hafla hiyo, alisema ziara hiyo itawapa walimu fursa ya kujifunza kwa vitendo badala ya kujifunza na kusoma kwa nadharia na kujionea ikolojoa nzima ya Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA).

"Hakika hii ni ziara yenye tija na ufanisi mkubwa. Tunaamini itasaidia si tu katika kuwaongezea ari ya kazi kwa walimu wetu, bali pia kuhakikisha kuwa wanakuwa mabalozi wazuri wa mradi mkubwa wa reli wa SGR unaotekelezwa na serikali," alisema.

Awali Meneja Uhusiano wa Benki ya NMB, Cuthbert Zimbwe wakati wa hafla hiyo, alisema uhusiano wa benki hiyo na walimu una historia ndefu huku akisisitiza dhamira ya benki hiyo kuendelea kutoa bidhaa na huduma zinazokidhi matakwa ya walimu.

"Tumekuwa na uhusiano mzuri na walimu kwa miaka mingi sasa. Ama kwa hakika, benki yetu ina historia ndefu na walimu. "Tunaamini mchango wetu katika ziara hii ya mradi wa SGR utasaidia kuweka tabasamu kwenye nyuso za walimu," Zimbwe alisema.



Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini, Dk. Charles Moses (kushoto), akikabidhi msaada wa vitanda 65 vyenye thamani ya Sh. milioni 29.9 kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kukabiliana na mlipuko wa kipindupindu. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# WHO yatoa msaada kukabili kipindupindu

**Na Grace Mwakalinga**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limetoa msaada wa vitanda 65 vyenye thamani ya Sh. milioni 29.9 kwa ajili ya kukabiliana na mlipuko wa kipindupindu nchini.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkazi wa WHO nchini, Dk. Charles Sagoe- Moses aliyekabidhi msaada huo jana katika ofisini za shirika hilo jijini Dar es Salaam, unalenga kupambana na magonjwa ya dharura, ikiwa ni pamoja na kipindipindu.

Alisema mlipuko wa kipindupindu ni tishio kwa sababu unaambukizwa na kusambaa kwa haraka nchi za Bara la Afrika na tangu mwaka 2021, milipuko ya mara kwa mara imeripotiwa maeneo mengi barani, ikiwamo Tanzania.

"Kwa mujibu wa ripoti ya hivi karibuni iliyotolewa na serikali, zaidi ya visa 4,000 vya ugonjwa wa kipindupindu na vifo zaidi ya asilimia 80 sawa na uwiano wa asilimia 1.9, vimeripotiwa tangu mlipuko wa ugonjwa huo kufikia Septemba 2023," alisema Dk. Sagoe.

Aliongeza kuwa WHO inatambua rasilimali kubwa inayohitajika katika kudhibiti kipindupindu na milipuko mingine ya magonjwa na wanapongeza serikali kwa juhudi zake endelevu za kudhibiti magonjwa ya milipuko katika mikoa iliyoathirika. Alisema WHO itaendelea kusaidia sekta ya afya nchini kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kama vile elimu kwa wataalamu wa afya na wananchi, pia kutoa vifaa tiba, magari na miongozo kutekeleza afua za afya.

Akipokea msaada huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu alisema WHO ni wadau wakubwa katika kuimarisha huduma za afya nchini, wakisaidia kuwajengea uwezo watoahuduma, pia utayari wa kupambana na magonjwa ya milipuko.

Alisema wizara imeweka utaratibu wa kupambana na magonjwa ya milipuko pindi yanaporipotiwa, akisisitiza msaada huo wa vitanda utasaidia kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu na vitawagiwa katika maeneo yenye uhitaji.

# Makamu wa Rais ataka hatua za kukabili mabadiliko ya tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewaelekeza watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais nchini kushirikiana na ofisi yake katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi Zanzibar.

Othman aliyasema hayo jana alipokutana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji aliyefika ofisini kwake kujitambulisha baada ya uteuzi wake uliofanyika hivi karibuni kushika wadhifa huo.

Alisema kuwa Zanzibar, hususani Pemba, imekuwa ikiathiriwa kwa kiwango kikubwa na maji ya chumvi kuingia katika makazi na mashamba ya kilimo na hivyo kuathiri mustakabali mzima wa maisha ya kila siku.

Othman alielekeza taasisi mbili za mazingira ambazo ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Baraza la Mazingira (ZEMA) kukaa na kutafakari kwa pamoja mbinu na hatua za kuchukua.

Dk. Kijaji aliahidi kutenga siku zake za kazi kila mwezi kukaa katika ofisi yake ya Zanzibar ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

Akizungumza na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) Hamza Hassan Juma, pamoja na mambo mengine, walikubaliana kuimarisha ushirikiano katika utendaji wao wa kazi.

Waziri Dk. Kijaji ameahidi ushirikiano kwa ofisi hiyo ili serikali zote mbili zihudumie wananchi kwa ujumla.

Waziri Juma aliahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote ya viongozi kutoka pande zote mbili za muungano na kumkaribisha wakati wote Waziri Kijaji anapohitaji kubadilishana uzoefu katika kuimarisha muungano huo.



# Mgombea urais TLS aahidi kupambana na 'vishoka'

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MGOMBEA nafasi ya urais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Sweetbert Nkula amesema kuwa ikiwa atachaguliwa kushika nafasi hiyo atahakikisha anafanyia kazi vipaumbele vyake vinne ikiwamo kukomesha vishoka katika taaluma hiyo.

Nkula, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi huo uliotarajiwa kufanyika jana kwenye mkutano mkuu wa TLS.

Alisema moja kati ya vipaumbele hivyo ni kukomesha wote wanaochafua taaluma ya mawakili aliowaita kuwa ni vishoka.

Aidha, vipaumbele vingine alivyovitaja ni pamoja na mawakili kuwa na mazingira bora ya utendaji wao kuanzia ngazi ya wilaya hadi mikoani ili kuwaletea maslahi mazuri pamoja na huduma za kiafya.

"Wadau wengine watakaokuwa na mahusiano kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa kazi ni pamoja na serikali yenyewe ili waweze kurudisha utaratibu wa kutoa kazi kwa mawakili serikalini hivyo nitajenga mahusiano mazuri na serikali yetu.

"Hii itatuwezesha kuiomba serikali kazi zote zinazohusiana za sheria zifanywe na mawakili kisheria," alisema.

Pia, Nkula alibaisha vipaumbele vingine kuwa ni kuimarisha mahusiano kati yao na mahakimu wa mahakama kwa kufanya kazi kwa kushirikiana kwa ufanisi zaidi.

Kipaumbele kingine alisema ni kufanya kazi na Jeshi la Polisi kwa kunzingatia kuwa wao ni wadau wakubwa kwa mawakili ili wafanye kazi kwa kushirikiana na kuheshimiana kati ya pande zote mbili.

Alisema wadau wengine ni Bunge ambao watahakikisha kuwa wanashirikiana katika kutunga sheria zinazohitajika kwenye katiba ya nchi ambayo kwa upande wa mawakili ni sehemu yao katika kuzingati sheria.

Alitaja wadau wengine ambao ni vyombo vya habari na wanajamii ambao kwa upande wa habari wanatoa elimu kwa jamii kuhusu sheria na kazi zinazofanywa na mawakili.

Katika kinyang'anyiro hicho cha kungombea urais wa chama hicho, wagombea wengine ni Boniface Mwabukusi, Kapteni Ibrahim Bendera, Emmanuel Muda, Revocatus Kauli na Paul Kaunda.

# Madiwani wawasilisha kilio cha wananchi gharama matibabu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
ITIGI

MADIWANI wa Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni mkoani Singida wamelalamikia gharama kubwa wanazotozwa wananchi wanapokwenda kupata huduma za matibabu ambazo zinatofautiana kwa kila kituo cha afya na zahanati.

Walitoa malalamiko hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani na kwa nyakati tofauti wamekuwa wakilalamikia gharama kubwa za matibabu hasa huduma ya mama na mtoto na HIV kutozwa fedha.

Walisema kwenye vituo vya afya baadhi vinatoza Sh. 7,000 na vingine Sh. 40,000 za papo kwa papo hali inayozua malalamiko kwa wananchi.

Diwani wa Viti Maalum, Elizabeth Kidolezi, alisema malalamiko hayo wameyafikisha mara kadhaa kwa Mganga Mkuu wa halmashauri na madiwani walishashuhudia kliniki tembezi zikitoza pesa kwa wananchi.

Naye Diwani wa Kata ya Rungwa, Said Yahaya, alisema kwenye maeneo kama Sikonge mkoani Tabora gharama inayotozwa ni Sh. 7,000, lakini kwenye halmashauri yao inaenda mpaka Sh. 40,000 kulingana na matibabu ya mgonjwa husika.

"Tunataka tufahamu tunatumia sera tofauti na Sikonge au sisi tunasera yetu? Sikonge wao wanalipa Sh. 7,000, lakini sisi papo kwa papo mgonjwa anaweza akalipa hata Sh. 35,000, 25,000 hadi Sh. 40,000 kulingana na matibabu ya siku hiyo," alisema.

Diwani wa Viti Maalum, Kata ya Mitundu, Rose Madunba, alisema pia gharama za upasuaji zimekuwa kubwa katika vituo vya afya vya halmashauri hiyo ikilinganishwa na halmashauri nyingine.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Husseni Simba, alihoji kuwa kama ni kuchangia kuleta vifaa vya upasuaji vinavyopungua kwanini gharama zitofautiane wakati upasuaji unaofanyika ni uleule.

"Tunataka tuelewe kiwango cha mtu anayefanyiwa upasuaji kwenye vituo vile anatakiwa atoe shilingi ngapi mana haieleweki, wengine wanalipa 70,000 wengine laki moja wengine laki mbili," alisema.

Akijibu malalamiko hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Itigi, Ayoub Kambi alisema kwa mujibu wa Sera ya Afya ya taifa huduma ya mama na mtoto pamoja na huduma ya HIV zinatakiwa zitolewe bila malipo.

"Sera kwa kinamama upasuaji ni bure kama kuna ulipishwaji naombeni nilichukue nilifuatilie kwenye vituo vyangu vya afya ili tujue wanalipishaje na kwanini wanalipisha na kwanini zinatofautiana, lakini mimi najua ni bure," alisema Kambi.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Itigi, Dk. Frederick Gaisha, alisema utofauti wa gaharama unatokana na hadhi ya vituo vya kutolea huduma ya afya ya lipa papo kwa papo na lipa kwa huduma kulingana na hadhi ya kituo au zahanati.

"Kuna sera ya lipa kwa huduma na kituo cha afya kinatumia sera ya lipa kwa huduma na hii sio kwa halmashauri ya Itigi tu ambayo ni tofauti na lipa papo kwa papo, lakini zahanati zetu zote mpaka sasa wanalipa papo kwa papo ya Sh. 10,000," alisema.



Baadhi ya Wakazi wa Jiji la Dodoma, wakiwaangalia wanyama aina ya ngamia na farasi, walipotembelea maonesho ya nanenane yanayofanyika katika viwanja vya Nzunguni, jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watakiwa kutumia vizuri fedha za miradi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Gugu, amewataka maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali Jeshi la Polisi kutumia vizuri fedha za miradi zinazotolewa na serikali ili ikakamilike kwa wakati.

Gugu, alisema hayo katika ziara yake ya kwanza tangu uteuzi wake makao makuu ya Jeshi la Polisi na kupokewa na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Camilius Wambura na baadaye kutembelea mradi wa nyumba za makazi ya askari polisi unaoendelea kujengwa jijini hapa.

"Tunapoanza utekelezaji wa bajeti katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, Jeshi la Polisi linatakiwa kuongeza viwango zaidi katika miradi yao pia kufanya maombi ya fedha za miradi hiyo kwa wakati ili iweze kukamilika kwa muda uliokusudiwa," alisema.

Aidha, Gugu alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kuendelea kutambua majukumu yao ya kulinda usalama wa raia pamoja na mali zao ipasavyo.

"Sisi kama wizara tunatambua kazi kubwa na adhimu ambayo mnaifanya na tutaendelea kuwapongeza kwa kazi nzuri mnayoendelea kuifanya hongereni sana," alisema.

Aidha, Gugu aliwataka watumishi wa Jeshi la Polisi kuendelea kuwa wazalendo na kuifanya kazi yao kizalendo kwa sababu nchi inapokuwa na amani na utulivu shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii zitaendelea vizuri.

"Hata pale Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, anapohamasisha utalii, hao watalii hawataweza kufanya shughuli zao za kiutalii ikiwa hakuna amani na utulivu," alisema.

Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camilius Wambura, alisema nchi ipo salama licha ya hivi karibuni kuibuka malalamiko ya watoto kufanyiwa vitendo vya kikatili pamoja na unyanyasaji dhidi ya kinamama na vyote vimeshughulikiwa.

Alisema Jeshi la Polisi limejiwekea utaratibu wa kufanya kazi kwa bidii, weledi na nidhamu ili wananchi wapate haki na matokeo mazuri ya kazi ya jeshi hilo nchini.





# Hospitali yaagizwa kununua kifaa kuchomea taka

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar ameuagiza uongozi wa Hospital ya Abdalla Mzee, Mkoani Pemba, ndani ya mwezi mmoja kununua mtambo mpya wa kuchomea taka za hospital ili kuepusha kusambaa kwa taka hizo ili kuepusha maradhi ya mlipuko.

Akikagua uendeshaji na utoaji wa huduma katika hospitali hiyo, Hemed aliutaka uongozi wa hospitali kujipanga kuhakikisha huduma zote muhimu zinapatikana hospitalini hapo kwa wakati unaostahiki.

Alisema kuwapo kwa mtambo wa kuchomea taka kutasaidia wafanyakazi kufanya kazi zao kwa ufanisi na kwa kiwango kilicho kusudiwa na serikali cha kuwapatia huduma bora za afya wananchi wote wa Unguja na Pemba.

Aidha, Hemed alisema amefarijika kuona huduma ya usafishaji wa figo (Dialysis), Ultrasound, X-ray na huduma nyingine za maabara zinapatikana bila ya malipo pamoja na dawa za kutosha kwa wagojwa wanaopatiwa matibabu hospitalini hapo jambo ambalo ndio dhamira ya Rais Dk Mwinyi.

Alimwagiza Afisa Mdhamini Wizara ya Afya kushughulikia kwa haraka maslahi na stahiki za wafanyakazi ili kuwapa moyo wa ufanyaji wa kazi kwa kuwapatia wagonjwa huduma bora bila ya usumbufu.

Wakati huo huo, alikagua mradi wa Shule ya Msingi Chanjaani Jombwe na Shule ya Sekondari Ole zinazojengwa na Mkandarasi Kampuni ya Mwinyi Building Contraction na Benchmark & Engineering Ltd ambazo zipo katika hatua za mwisho kukabidhiwa kwa serikali.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeamua kuekeza katika sekta ya elimu kwa kuhakikisha inaweka miundombinu bora ya elimu ili wanafunzi wasome katika mazingira mazuri yatakayotoa wataalamu wabobezi wa fani mbalimbali ambao watalisaidia taifa kufanya kazi ndani na nje ya nchi.

Hemed aliwataka wazazi na walezi kulipa kipaumbele suala la kuwapatia elimu bora watoto wao pamoja na kuwalea katika maadili mema.

Naye Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulghulam Hussein, alisema malengo ya serikali kupitia Wizara ya Elimu ni kuhakikisha inakamilisha miradi yote inayojengwa, kuongeza idadi ya madarasa na kujenga dahalia za kisasa ili ifikapo Januari 2025 wanafunzi wote wanaingia mkondo mmoja wa masomo.

Wakandarasi wanaojenga miradi hiyo walisema wapo katika hatua za mwisho kukamilisha ujenzi huo na wanatarajia kuikabidhi serikalini mwishoni mwa mwezi huu ili wanafunzi waendelee na masomo yao katika mazingira mazuri na salama. Miradi iliyokaguliwa na Makamu wa pili katika ziara yake hiyo ni Hospital ya Abdalla Mzee Mkoani, ujenzi wa Shule ya ghorofa Mwambe, ujenzi wa barabara ya Ukutini mtangani, ujenzi wa soko la samaki na mboga Vitongoji, ujenzi wa kituo cha kuchomea taka vitongoji na kukagua maendeleo ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Ole Mkoa wa Kusini Pemba.

# ‘Sheria Tanzania zizingatie usawa kijinsia kwenye uamuzi’

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amesema ni vyema kufanyike uchambuzi wa kina kwa sheria za Tanzania bara na Zanzibar ili usawa wa kijinsia upatikane na kufikia asilimia 50 kwa 50 baina ya wanaume na wanawake kwenye ngazi za maamuzi.

Waziri huyo alisema sheria zilizopo sasa ni za zamani ambazo zilitungwa baada ya uhuru Tanganyika na Mapinduzi na wakati huo zilimpa nafasi kubwa mwanamume katika mambo mbalimbali na hatimaye mwanamke kuachwa nyuma.

Akizungumza jana katika mkutano wenye lengo la kujadili kuunganisha usawa wa kijinsia katika kutunga sheria kwa ajili ya kuangalia mikakati ya kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, uliofanyika visiwani Zanzibar, alisema nafasi za kushiriki wanawake katika uongozi zipo, lakini sheria zilizopo zinahitaji kufanyiwa maboresho ili kulinda haki za wanawake.

Alisema mwamko uliojengwa miaka ya nyuma kupitia mikutano mbalimbali ya kimataifa ya kupigania usawa wa kijinsia, unapashwa kuendelezwa ili uhuru wa kijinsia utawale katika kila kitu.

Mtaalam wa mradi wa kutokomeza ukatili wa kijinsia, kutoka Shirika la Kimataifa la Kusaidia Wanawake (UN WOMEN), Lucy Tesha, alitoa muhtasari wa sheria ya mapendekezo na kusema uchambuzi huo unatoa mapendekezo 76 yanayohusiana na jinsia katika sheria zote zilizopitiwa.

“Inabainisha kuwa jumla ya sheria mbili lazima zifutwe kabisa, sheria 18 zibadilishwe au zirekebishwe, na sheria tano za habari zichukuliwe ili kuleta mfumo wa kutunga sheria wa Tanzania Bara na Zanzibar katika kikanda na kimataifa,” alisema.

Tesha alisema, licha ya mpango wa kisheria na kisera unaofanywa na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwapo kwa upungufu wa kijinsia kutahusisha utashi madhubuti, uongozi wa kitaasisi mfumo wa mageuzi wa kisheria na kuongeza rasilimali.

Alisema hasa ukiukaji wa sheria hizo ni kikwazo kikubwa cha kufikia usawa wa kijinsia, ambazo ni Sheria za ubaguzi zinazuia kufurahia kikamilifu haki za kiuchumi, kijamii, kitamaduni za kiraia na kisiasa.

Pia, alisema sheria na vifungu kadhaa vya sheria lazima virekebishwe Tanzania Bara na Zanzibar ili kuhakikisha usawa wa kijinsia na Katiba, inapaswa pia kufanyiwa marekebisho ili kujumuisha ufafanuzi unaoendelea unaoshughulikia sheria na utendaji na kutumika kama msingi wa haki za wanawake katika nchi.

Aidha, alisema Tanzania Bara sheria 11 zinapaswa kurekebishwa au kufutwa ni kama vile sheria ya umri wa chini wa kuolewa kwa wavulana na wasichana, kuondoa lugha zenye upendeleo wa kijinsia katika sheria za uchaguzi, na kwa Zanzibar sheria saba ikiwamo sheria za uchaguzi kurekebishwa, sheria ya unyanyasaji dhidi ya wanawake inapaswa kuwekwa wazi jambo ambalo linaweza kuongeza usawa wa kijinsia.

Naibu Katibu Mkuu wa Shule ya Sheria Zanzibar, Msemo Mavare, alisema kuwa hicho ni kikao kinachojadili suala la kufanya marekebisho na kutunga sheria zitakazomwezesha mwanamke kuendeleza kwa vitendo kaulimbiu ya mwanamke kushika uongozi na maamuzi ya kitaifa, pamoja na malengo yaliyowekwa na katiba ya sheria kufikia asilimia 50 kati ya wanamume na wanawake.

“Wanawake wanawakilishwa katika maeneo mengi ya uongozi, hata hivyo, bado hatujafikia uwiano sawa. Mfano mzuri ni wawakilishi, wabunge na sisi kama wanasheria tumekuja kuunga mkono hili kwa kutoa mwongozo,” alisema.



Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Hassan Kaduara akikagua mita ya umeme katika eneo la Chuwini, nje ya mji wa Zanzibar juzi, baada ya kupata taarifa ya wizi wa umeme kwa mmoja wa wafanyakazi wa shirika la umeme. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mfanyakazi ZECO adaiwa kuwaunganishia umeme ndugu bila utaratibu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduara amesikitishwa na kitendo kilichofanywa na mtu anayedaiwa kuwa mfanyakazi wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), kuunga umeme kinyemela na kuwasambazia ndugu zake.

Waziri Kaduara alilibaini hilo jana wakati akiwa katika ziara yake ya kukagua miundombinu ya umeme huko Chuwini nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema mfanyakazi huyo, Mwinshaa Juma Kheri, aliiba umeme kwa kuifanya mita ya nyumba yake kutosoma kiwango cha matumizi, lakini pia kuunga umeme kwa nyumba nyingine tano bila ya utaratibu.

Alisema baada ya kufuatilia tukio hilo alibaini kuwa watu hao aliowaungia umeme wote walikuwa ndugu zake wa familia moja jambo ambalo halikubaliki kisheria na linaikosesha serikali mapato.

“Tukio hili kwa kweli haliwezi kuvumilika na hawa wote tutawakamata na kuwapeleka katika vyombo vya sheria, kila siku tunapiga kelele kuhusu wizi wa umeme lakini leo mfanyakazi wa ZECO, ambaye anatakiwa kuwa mlinzi wa kwanza yeye ndiye anahujumu na kuwasambazia umeme ndugu zake inasikitisha,” alisema Waziri Kaduara.

Aidha, alisema kwa hatua ya awali alizochukua alilitaka jeshi la polisi kuwakamata na kufanya uchunguzi na mfanyakazi huyo kusimamishwa kazi na taratibu zingine za kiutumishi zitaendelea.

Aliwataka wananchi kuacha abia ya kujiungia umeme kinyume na utaratibu na hakuna sababu ya kufanya hivyo, hasa baada ya serikali kupunguza gharama za kuunga umeme kutoka Sh. 400,000 mpaka 200,000.

Mkurugenzi wa Nishati na Madini, Saidi Mdungi, alisema idara itaendelea na opereshini za kuwasaka wezi wa umeme na wanaotumia vibaya miundombinu ya nishati hiyo na wakibainika watachukuliwa hatua za kisheria.

Aidha, awaliwataka wafanyakazi wa ZECO kuanza kujitathmini wenyewe kabla ya idara kuwakagua wafanya kazi wote wa ZECO na atakayebainika kuhujumu miundombinu, atachukuliwa hatua ili kuhakikisha wafanyakazi wanatumia umeme kihalali.


Sheha wa shehia ya Chuini, Shaaban Abdalla Suleiman, alisema kitendo kilichofanywa na mfanyakazi huyo kutoka shehia yake kimeichafua shehia na kuwakata wananchi wa shehia hiyo kuacha tabia ya kujiungia umeme kinyume na utaratibu.



**MR BLUE**

UKURASA 13

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI AGOSTI 3, 2024



# MAHABA YALIYOPITILIZA

MWANAMUZIKI na mwanamitindo, Hamisa Mobetto, ameibua gumzo katika tuzo za wanasoka bora zilizofanyika juzi jijini Dar es Salaam, baada ya kuonyesha hadharani mahaba mazito kwa mchezaji wa Yanga Aziz Ki.

Katika sherehe ya tuzo hizo zilizoandaliwa na shirikisho la soka nchini (TFF), Hamissa alionekana kivutio kutokana na kile kinachoelezwa mapenzi yaliyopitiliza mchezaji huyo ambaye wakati fulani alionekana akimfuta machozi.

Hamisa na Azizi Ki, walionekana kama wamezaliwa upya kwa kile walichokuwa wakikifanya jukwaani na huku wakishangiliwa na watu waliohudhuria.

Hata Hamisa alipoulizwa kama anaweza kwenda pamoja na Aziz Ki Dubai kwa mapumziko ya siku nne, mrembo huyo hakusita kujibu ndio na kusababisha ukumbi mzima kurindima kwa furaha.

Watu waliokuwepo ukumbini walibaki midomo wazi pale Aziz Ki, aliposhindwa kuamini kama Hamisa anaweza kufanya mambo yote hayo hadharani na kubaki akitoa machozi.

"Aziz Ki kazidiwa na mahaba amekuwa kama mtoto  mdogo, kweli Hamisa anajua kupenda na kumfanya mwanaume kuchanganyikiwa," amesikika mmoja wa watu waliokuwa ukumbini.

Wawili hao wamekuwa katika uhusiano wa kimapenzi kwa miezi kadhaa sasa, na wakati mwingine wameonekana wakiambatana katika shughuli mbalimbali za kijamii.

**BASI SAWA**

## Snura hataki kukumbuka ya nyuma




ALIYEKUWA msanii wa muziki, Snura, ambaye ametangaza kuachana na Sanaa, amesema kwa sasa amesitirika na hataki kujihusisha na matukio ambayo yanaweza kuathirika.

Amesema baada ya kumrudia Mungu, hawezi kukumbuka matukio ya nyuma ikiwamo kuposti picha katika mitandao ya kijamii kwa sababu anahisi anaumia.

"Maisha yangu yamebadilika, nimetoka kule nilipokuwa na sasa naishi katika njia ya haki ambayo naamini inanipa furaha," amesema Snura.

## Johari atambia mafanikio



MWIGIZAJI na mtayarishaji wa filamu, Johari, amesema ilikuwa vigumu kwake kusimamia utengenezaji kama mwanamke, lakini amefanikiwa kutokana na kujiamini na ujasiri.

Amesema kuwa kwa hatua aliyofikia hawezi kuangushwa na maneno ya watu kwamba kuna watu wanazibeba kazi zake, bali ataendelea kujikita katika safari yake kwa kuongeza ubunifu na ubora katika kazi zake.

"Watu wakisema kwamba napendelewa hilo haliwezi kuniyumbisha, kitu ambacho watu hawakielewi ni kuwa katika safari yangu ya kisanaa mimi ndiye mwanamke wa kwanza kuongoza filamu na watu wakakubali kazi yangu," amesema Johari.



## STARSHINE AWAZUNGUMZIA DIAMOND, MARIOO

Mashindano ya nyimbo mbili za wasanii, Diamond Platnumz (Komasava) na Marioo (Hakuna Matata) zimemuibua msanii kinda wa Bongo Fleva, Starshine aliyevutiwa na ukubwa wa ngoma hizo.

Akizungumza na BT jana, Starshine alisema kwa sasa hakuna msanii mwenye nguvu kama Diamond Platnumz hivyo wasanii wengine wasishindane naye kwa kutoa wimbo pamoja kama alivyofanya Marioo, japo ushindani ni mzuri kwenye muziki.

"Marioo na wimbo wake Hakuna Matata amejitahidi sana kupambana na wimbo wa Komasava ya Diamond, ila amepotezwa vibaya, ilitakiwa asitoe wimbo kwenye kipindi hiki ili wimbo wake usikike zaidi. Mimi Starshine niliacha kutoa wimbo kipindi kile nikimpisha Diamond ila mwezi huu mapema nitaachia wimbo wangu unaitwa Danga na ninaamini utafanya vizuri," amesema Starshine.



## Mr Blue na kisa chake...

MSANII mkongwe wa muziki wa kizazi kipya, Mr Blue, amekumbuka jinsi alivyotolewa nje ya studio ili kumpa nafasi Juma Nature, kuingiza sauti katika wimbo wake wa kwanza.

Amesema toka alipokuwa mtoto amekuwa mfuasi sugu wa Nature hivyo aliamua kumtafuta kwa ajili ya kutimiza ndoto yake ya kuimba pamoja.

"Nilimtafuta kaka Nature twende akaingize sauti katika wimbo wangu wa kwanza, lakini tulipofika pale studio mimi nilitolewa nje ili kaka aweke sauti. Licha ya kuumia mimi niliyemleta nimetolewa nje lakini nilifurahi jinsi kaka alivyopasuka na kujiona nina bahati," amesema.

## WASANII, WANAMUZIKI NDUGU

**Na Adam Fungamwango**

KWA asilimia kubwa kipaji huwa hakirithishwi. Kipaji ni uwezo na karama inayotoka kwa Mungu kwenda kwa binadamu mmoja pekee. Hata hivyo mara chache hutokea, watoto kurithi vipaji vya baba zao. Hata hivyo ni lazima kutakuwa na utofauti. Mmoja wapo, baba au mtoto atakuwa juu kuliko mwenzake.

Pia hutokea mara chache ndugu wa kuzaliwa kuwa na kipaji cha aina moja. Wanaweza kuwa waigizaji, wanamuziki, wachoraji, au wanamichezo.

Huko nyuma kulikuwa na ukoo wa kina Kihwelo. Mussa Kihwelo, Mwesa Kihwelo, Mtwa Kihwelo, Jamhuri Kihwelo, Muhehe Kihwelo na wengine, wote hao wakiwa ni wacheza soka.

Kulikuwa na Kitwana Manara, Sunday Manara na Kassim Manara. Kwa upande wa muziki hasa wa nje ya nchi kwa vijana wa sasa kuna mapacha walioinda kundi la P-Square ambao ni Peter Okoye na Paul Okoye.

Hapa Tanzania wanandugu ambao wamekuwa na vipaji vya muziki na kuwa maarufu sana tangu enzi hizo mpaka sasa.

### Familia ya kina Uvuruge

Kama Tanzania imewahi kupata wanamuziki wengi kutoka kwenye familia moja kama ilivyokuwa kila Kihwelo kwenye soka, basi ni ukoo wa kina Uvuruge.

Ni familia maarufu sana kwenye muziki wa dansi tangu miaka ya '70. Hao ni kila Jumanne Uvuruge, Khalfan Uvuruge, Uruka Uvuruge, Maneno Uvuruge na Fadhili Uvuruge.

Ni wanamuziki wa familia ya wanamuziki wakubwa kabisa nchini, waliopata heshima kwa uwezo mkubwa wa kupigia bendi mbalimbali nchini.

Jumanne ndiye mtunzi wa wimbo maarufu sana nchini wa Safari Trippers 'Georgina' ambao hakuna 'live' yoyote ya bendi itanaliza muziki bila kupiga wimbo huo.

### Ezekiel Mazanda na David Mazanda

Hawa ni wanamuziki waliokuwa mapacha. Wote walikuwa wanapiga gitaa la kati 'rhythm'.

Waliwika sana mwanzoni mwa miaka ya '80 walikuwa kwenye bendi mbili tofauti.

Ezekiel, alikuwa ni mwanamiziki wa bendi ya Urafiki Jazz, huku pacha mwenzake David akiwa ni mwanamuziki za bendi ya Bima Lee. Wote wamefariki dunia kwa nyakato tofauti.

### Wilson Peter na George Peter

Ni wanamuziki ndugu ambao ni maarufu zaidi kwenye muziki wa dansi si Tanzania tu, bali Afrika Mashariki. Vijana hawa Watanzania kutoka Hale mkoani Tanga, walikuwa wanamuziki wa Jamhuri Jazz Band, kabla ya kujiengua na kuunda bendi ya Arusha Jazz, baadaye ikavuka mpaka na kuingia nchini Kenya ambako waliibadilisha jina la kuita Simba Wanyika.

Wilson ambaye ni mkubwa, yeye ndiye alikuwa kiongozi, akipiga gitaa la solo, akiimba sauti ya kwanza, huku mdogo wake George ambaye aliimba sauti ya pili na ya tatu, sauti ambayo iliigwa na Tx Moshi William baadaye. Wakati Geogre akifariki mwaka 1992, kaka yake Wilson alifariki mwaka 1995, wote wakizikwa nchini Kenya.

### James Kibosho na Martin Kibosho

Akina Kibosho ni wapiga drums maarufu sana nchini, wakiwa wamepitia bendi mbalimbali kama vile Extra Bongo, Twanga Pepeta na bendi mbalimbali za muziki wa dansi wa kisasa.

James na Martin Kibosho ambao ni mtu na mdogo wake, ni moja kati ya familia chache nchini ambazo zimetoa ndugu wenye kipaji cha aina moja na hadi leo wanaendelea na muziki kwenye bendi mbalimbali nchini.

### Ali Kiba na Abdul Kiba

Naweza kusema kuwa, familia hii imebarikiwa, kwani pamoja na kwamba wote wawili wana uwezo mkubwa wa kucheza soka na ushuhuda ulionekana kwenye mechi dhidi ya 'team Kiba na team Samatta' hivi karibuni, lakini wote pia ni wasanii maarufu wa muziki wa bongo fleva.

Ali na Abdul kila mmoja anafanya kazi kivyake, kila mtu akitoa ngoma yake kwa wakati wake, na wamekuwa wakilitikisa soko la muziki wa kizazi kipya. Ni wasanii wa viwango cha juu kabisa nchini kwa sasa.

**FILAMU**

## Ndoano imewachoma

**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA siri ya watu wawili duniani. Siri pekee ambayo inaweza kusitirika ni ya mtu mmoja.

Hili ndilo linajitokeza kwenye filamu hii ya 'Ndoano'. Stanley Msungu ndiye kinara wa filamu hii.

Msungu na mkewe wanaishi kwa amani na utulivu katika ndoa yao iliyojaaliwa kupata mtoto mmoja wa kike aitwaye Suzan.

Siku moja binti yao alitoweka nyumbani, Msungu akamtafuta na kumkuta na jamaa mmoja wakiwa dukani akinunuliwa vitu. Kabla hajafanya chochote, anatoweka na mtoto. Anampigia simu mkewe na kumueleza wajihi wa mtu aliyemkuta na mtoto wao. Mkewe anashtuka.

Wiki moja baadaye mtoto anatekwa na watekaji wanampigia simu baba yake wakihitaji jumla ya Sh Milioni 10. Kazi ya kuzitafuta pesa hizo inachukua muda, lakini zinapatikana na mtoto anarudi nyumbani.

Miezi kadhaa tena mtoto anatekwa na zinatakiwa Sh Milioni 5. Nani anayefanya kazi hii? Kwa nini? Na chanzo ni nini?

Baada ya kukaa miaka kadhaa bila kupata mtoto, mke wa Msungu alikuwa na wasiwasi na ndoa yake. Shoga yake akamwambia aende hospitali kupima ili kuonekana kama ana matatizo. Hakuonekana nayo, hivyo moja kwa moja mwenye mapungufu atakuwa ni mumewe.

Kwa ushauri wa shoga yake ni kwamba asimwambie mumewe, bali amtafute mwanaume mwingine ampe mimba na mtoto ambambikie mumewe. Anatafutwa mwanaume mmoja anaitwa Julio. Anaifanya kazi yake ipasavyo kwa mkataba wa kulipwa pesa.

Hivyo ndivyo mtoto Suzan alivyopatikana.

Ni Msungu tu ambaye hajui kinachoendelea. Julio analipwa Sh Milioni 5, zingine zinachelewa na jamaa alipotishia kutoa siri, mama anafanya kila njia analipa.

Tamaa ya pesa inawaingia Julio na shoga wa mke wa Msungu ambao ndiyo wenye dili hizo.

Wanaamua sasa kuwa baada ya muda wanamteka mtoto kwa ajili ya kujipatia pesa.

Msungu haelewi ni kwa nini mtoto wake anatekwa, mkewe analifahamu hilo na mara kwa mara anawaonya Julio na shoga yake juu ya tabia hiyo, lakini wanatishia kutoa siri.

Mke wa Msungu mambo yakamtokea puani na sasa akawa hana amani ya ndoa. Muda wote mambo yanaweza kuharibika.

Anaamua kutafuta kundi ya wauaji kwa ajili ya kumuua Julio ili kunusuru ndoa. Hilo linafanyika.

Baada ya kuona Julio amefariki, shoga wa mke wa Stanley naye akaona yanaweza kumfika na yeye, akaamua kujiua mwenyewe. Hapo ndipo amani na furaha kwenye ndoa ya Msungu na mkewe ikapatikana.





# Qing aikingia kifua Benin

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Qing Madi amefunguka kuhusu maisha yake akiwa nchini Benin, akisema yalitawaliwa na utulivu na upendo.

Madi akiwa katika kipindi cha 'Is This Seat Taken', amesema tofauti na watu wanavyoitaja Benin, lakini akiwa mtoto aliishi maisha mazuri akiwa huko.

"Ni ya amani; najua maneno yake mafupi. Benin sio jinsi watu wanavyoichora ina amani na kila mtu anamjua mwenzake," ameeleza.



## Kumbe Meghan alivumilia mengi

KATIKA sura mpya ya sakata linaloendelea ndani ya familia ya kifalme ya Uingereza, imefichuka kuwa Prince William alidaiwa kumpiga marufuku Meghan Markle kuvaa vito vya Princess Diana.

Dai hilo linatokana na kitabu cha Robert Jobson ambacho kitachapishwa hivi karibuni, kinachoitwa Catherine, Princess of Wales: Wasifu wa Malkia wa Baadaye.

Kitabu hicho kinadai kuwa katika siku za mvutano kabla ya harusi ya Prince Harry na Meghan, Prince William alitafuta uhakikisho kutoka kwa Malkia Elizabeth II kwamba Meghan hatavaa vito vyovyote vya Diana.

## R. Kelly kutupa kete ya mwisho

MWIMBAJI mkongwe wa R&B, Robert Kelly maarufu kama R Kelly, ambaye kwa sasa anatumikia kifungo gerezani, amuamua kucheza karata yake ya mwisho kutaka kuwa huru.

Mwanamuziki huyo amekata rufaa mahakama ya juu ya Marekani akitaka kubatilishwa hukumu aliyopewa kutokana na mashtaka ya unyanyasaji wa kingono.

Julai 31, timu ya wanasheria wa Kelly iliwasilisha rufaa mahakamani, ikitaka kubatilisha hukumu ya msanii huyo mwenye utata, ambaye anajulikana kwa vibao kama vile, I Believe I Can Fly.

R Kelly alihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela mwaka wa 2022 baada ya kupatikana na hatia ya unyanyasaji wa kingono kwa watoto wadogo, utumwa na ulaghai.





## Vybz awatia wasiwasi mashabiki

STAA wa nyimbo za Dancehall kutoka Jamaica, Adidja Palmer maarufu Vybz Kartel na washtakiwa wenzake watatu waliachiliwa kutoka gerezani kwa uamuzi uliotolewa na Mahakama ya Rufaa ya nchi hiyo.

Amekuwa gerezani tangu 2011 baada ya kupatikana na hatia ya mauaji ya Clive "Lizard" Williams.

Wakati wa kuachiliwa kwake, alikutana na umati wa wafuasi ambao walimshangilia wakati akitoka gerezani. Hata hivyo, alikuwa amevaa miwani ya jua na kanga ili kuficha uso wake.

Hata hivyo baadaye, picha na video za msanii huyo ziliibuka zikionyesha jinsi uso na shingo yake ilivyovimba, jambo ambalo lilizua wasiwasi miongoni mwa mashabiki wake.

Inaripotiwa kuwa nyota huyo wa dancehall amekuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa Graves na ugonjwa wa moyo, ambao ulisababisha kuachiliwa kwake.

## KRG, Otile jino kwa jino

MWANAMUZIKI wa Kenya, KRG the Don, amesema msanii mwenzake Otile Brown ni mbinafsi na hajui kuwajibika.

Wasanii hao wapo kwenye ugomvi baada ya Otile, ambaye alimtaja mwanamuziki huyo kuwa hawezi kumfikia kiwango chake.

"Otile ni mtu mwenye ubinafsi. Bien ametoa watu wangapi? Amefanya kolabo na wasanii wengine wadogo, wakainuka. Mimi sipendi mtu ambaye anatumia watu kwenda juu, wakati yeye anarudi nyuma," ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram.



# Wadau utalii washauri benki kuingia ubia SGR

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WAENDESHAJI wa utalii na wafanyabiashara mbalimbali wa Mkoa wa Arusha, wameipigia chapuo, Eco Bank (The Pan African Bank), wakiitaka kuingia ubia na serikali kwa uwekezaji wa reli ya kisasa ya SGR kutoka Dar es Salaam/ Tanga/ Moshi hadi Arusha, ili kufungua milango ya kiuchumi kwa sekta hiyo kaskazini mwa Tanzania.

Kwa sasa, Shirika la Reli nchini (TRC) linapambana kuhakikisha ujenzi wa sehemu zote za SGR unakamilika ifikapo mwaka 2028 ili wawekezaji watumie fursa hiyo na kutoa mchango mkubwa wa kukuza uchumi wa nchi.

Akizungumza jana jijini hapa katika mkutano wa wadau wa utalii na wafanyabiashara wanaofanya biashara na Eco Bank, Mshauri Elekezi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), anayehusika katika mchakato wa kutafuta wawekezaji wa ujenzi wa SGR, Peter Msumari, alisema kama Eco Bank watajitosa kuwekeza watasaidia kupanua sekta ya uchukuzi na kuwa miongoni mwa kampuni saba, ambazo zimeonyesha nia ya kushirikiana na serikali katika kuendesha Reli ya Standard Gauge (SGR).

"Nimekuwa nikitumiwa na serikali, kwa ajili ya kutafuta wawekezaji. Kwa sababu ni mradi mkubwa, ambao utawatoa Watanzania wengi kwenye umasikini kwa hiyo unapozungumzia sekta ya usafirishaji ni roho ya uchumi. Ni sekta ambayo huwezi kuikimbia, ukitoa maharage shambani lazima unahitaji usafiri kuyaleta mjini. Kwenye ripoti ambayo ilikwenda Benki ya Dunia (WB), tumewagusia pia na wawekezaji wengine ambao wangeweza kuwekeza kwenye SGR na wengine wamekubali."

"...Eco Bank nimewashauri kama wanaweza kuwekeza kwenye SGR waingize mkono wao haraka, kwa sababu ina mvuto kimataifa. Serikali haiwezi kufanya yenyewe kwa sababu kutoa reli kutoka Mkoa wa Pwani kuja Tanga, Moshi mpaka Arusha, na kwenda hadi Kigoma na Musoma, SGR ni mradi mkubwa wa matrilioni ya fedha."

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya Uendeshaji Utalii ya Kibeta Tours & Safaris, Edwin Mushumbusi, akizungumza katika mkutano huo, alisema wameishauri benki hiyo kuangalia namna ya kuwanyanyua kiuchumi, waendeshaji wadogo wa utalii kwa kuwapa magari ya kubeba watalii ili waepuke kukodi magari hayo kwa gharama kubwa. "Nikiwa kama mdau wa utalii, tumeishauri ni namna gani itatusaidia sisi wajasiriamali wa utalii namna ambavyo tutakua kiuchumi na kibiashara. Tumekubaliana na Eco Bank, kwamba inatuandalia mpango mahsusi kwa ajili ya kutupa mikopo ya magari ya utalii.

"Hayo magari yatatusaidia kupeleka wageni wetu katika vivutio mbalimbali vya utalii kama Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Geo Park."

Alisema waendesha utalii wadogo wanalazimika kukodi magari ya utalii na wakati mwingine wanapoteza fedha nyingi kwa ajili ya kukodi magari, lakini gari linapokuwa ni la kwako, unapata faida maradufu.

Akijibu hoja za wadau hao, Mkurugenzi Mkuu wa Eco Bank Tanzania Limited, Dk. Charles Asiedu, alisema wanapaswa kufanya zaidi katika sekta ya utalii, kwa kuwa benki hiyo iko katika masoko 33 ya Afrika.

"Tumeunga mkono SGR kwa usahihi, tuna uwekezaji kwa namna moja au mbili na washirika wetu. Arusha ni Jiji muhimu sana kwa Benki ya Eco. Kwa hivyo kwa nini tuna tawi hapa; pengine ni tawi kwa madhumuni ya kuhudumia soko. Hii ni kutokana na umuhimu wa sekta ya utalii nchi ya Tanzania leo."

## Wafugaji wajengewa mazizi kuzuia wanyama wakali

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WAFUGAJI wanaoishi ndani ya eneo la Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Burunge (Burunge WMA) wilayani Babati, Mkoa Manyara na jirani na maeneo hayo, wamejengewa mazizi ya waya (Boma Hai), ili kuzuia wanyama wakali hasa simba na fisi kuvamia na kula mifugo nyakati za usiku.

Mazizi hayo, yamejengwa na Taasisi ya uhifadhi na Utalii ya Chem Chem, ambayo inafanya shughuli za uhifadhi na utalii katika eneo hilo, lilipo kati kati ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa taasisi hiyo, kupunguza migogoro baina ya wanyamapori na mifugo.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi mazizi hayo, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara, Lazaro Twange, alisema mradi wa ujenzi mazizi hayo ni utekelezaji wa maagizo ya serikali kupunguza migogoro baina ya wanyamapori na binadamu.

Twange ambaye aliwakilishwa katika uzinduzi wa mazizi hayo na Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati, Khalfani Malipula, alisema kazi nzuri ya uhifadhi imefanyika na sasa kuna changamoto ya wanyamapori kula mifugo, jambo ambalo limeanza kupatiwa suluhu.

Alisema uzinduzi wa mazizi hayo, ambao umeambatana na maadhimisho ya siku ya askari wa hifadhi duniani (Rangers Day), unatarajiwa pia kuwaondolea wananchi adha ya kulala nje kulinda mifugo yao.

John Bagary, mkazi wa Kijiji cha Vilima Vitatu, alisema hadi juzi ng'ombe wake watano na mbuzi wanane walikuwa wameliwa na simba.

"Nimekuwa nikilala nje kulinda zizi langu la ng'ombe na mara kwa mara simba wanafika hapa usiku, lakini sasa nashukuru kujengewa zizi lenye uzio la taa la mwanga wa jua, ili kuzuia simba kuruka na kuingia ndani," alisema.

Mkazi wa Kijiji cha Ngoley, Peter Martin alishukuru Chem Chem na serikali kuwajengea mazizi hayo, ambayo yatawasaidia kulala kwa amani.

Msimamizi wa miradi ya maendeleo ya Jamii ya Chem Chem, Napendaeli Wazoeli, alisema Chem Chem kwa kushirikiana na askari wanyamapori, waliona katika maadhimisho ya siku ya askari wa wanyamapori duniani, wakabidhi mazizi hayo.

Alisema kila zizi limekuwa likigharimu zaidi ya Sh. milioni 2.6 na hadi jana mazizi 15 yalikuwa yamejengwa na taasisi hiyo, ili kukabiliana na migogoro baina ya wanyamapori na binadamu. Katika maadhimisho hayo, Chemchem walitoa vifaa vya kufukuza wanyama katika makazi ya watu, zikiwamo baruti, vuvuzela, pilipiki na tochi maalum za kufukuza wanyamapori.

Mwenyekiti wa Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori Burunge WMA, Erick Lilayoni, alisema hifadhi hiyo, itaendelea kushirikiana na Chem Chem na wadau wengine ili kuhakikisha hifadhi inaendelea kuwa kivutio cha watalii.

"Leo tumeona askari wote wanaolinda hifadhi hii wamepewa medali na vifaa vya kufukuza wanyamapori , sisi tunaamini huu ni mwendelezo tu Chem Chem kusaidia uhifadhi katika eneo letu," alisema.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Fakii Lulandala (katikati) akikagua muhogo aina ya kiroba kutoka kata ya Mutuka ambapo ekari moja inapandwa miche 4,000 na kupata tani 40, alipotembelea banda la Halmashauri ya Mji wa Babati, wakati wa maonyesho ya kilimo ya nanenane Kanda ya Kaskazini katika viwanja vya Themi Njiro, jijini Arusha juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Wasomi wajadili uhusiano wa vyuo, vyama vya ushirika

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WASOMI na watendaji kutoka mataifa mbalimbali duniani, wamejifungia kwa siku tatu katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), wakijadili uhusiano muhimu kati ya vyama vya ushirika na maendeleo endelevu.

Katika mkutano huo, wanapitia machapisho 50 ya wanazuoni na kuja na mikakati itakayosaidia kuboresha utendaji katika vyama vya ushirika, kuboresha sera, mipango iliyopo na kutafuta njia bora ya kutatua changamoto kwenye sekta ya ushirika.

Akitoa taarifa kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda kuhusu mkutano huo, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Prof. Alfred Sife, alisema mkutano huo unaofanyika kati ya Julai 31 hadi Agosti 2, mwaka huu, umeandaliwa na chuo hicho kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika Kenya.

"Kama tunavyojua sote, ajenda ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030 kuhusu maendeleo endelevu, inatambua jukumu muhimu ambalo mashirika ya binafsi (hasa vyama vya ushirika) vinatekeleza.

"Ajenda hiyo inatoa wito kwa vyama vya ushirika, kuongeza ubunifu na uvumbuzi wao katika kutatua changamoto endelevu na kuendeleza utekelezaji wa ajenda hiyo."

Mkutano huo unawashirikisha wanazuoni watendaji mbalimbali kutoka mataifa ya Tanzania, Kenya, Botswana, Ethiopia, Nigeria, Eswatini, Finland na India.

Aidha, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Kenya (CUK), Prof. Ngamau Kamau, alisema mkutano huo unalenga kujenga uwezo, kuja na mbinu bora, kushughulikia changamoto za kimataifa na kuwezesha jamii.

Wakati, Mwenyekiti wa mkutano huo, Prof. Mangasini Katundu, alisema wanapitia na kuchambua hotuba kuu sita na mawasilisho 50 kutoka kwa wanazuoni mashuhuri duniani kote.

Akizungumza na wasomi na watendaji hao, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, alisema tija ndogo katika kilimo cha mazao, haiwezi kumalizwa na sekta ya ushirika pekee, badala yake unahitajika kufanyika utafiti wa namna bora ya kulima na kuongeza tija.

Prof. Claudia Sanchez, alichagiza mada kuhusu uhusiano kati ya vyama vya ushirika na maendeleo endelevu yenye maarifa kutoka kwa mataifa yaliyochaguliwa ya Amerika na Ulaya, wakati Dk. Argan Wekesa na Beatrice Kimaro, waliendesha mjadala kuhusu utawala bora wa vyama vya ushirika na maendeleo endelevu.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Kisa cha mwanamuziki aliyeuawa kwa mapanga sababu ya nyumba ndogo

**Na Adam Fungamwango**

KUOA tunaona lakini tukumbuke yaliyotendeka kwa George Mukabi, George alipooa bibi akakimbia, kwa kumfuata akauawa bure. Wazazi wa Mukabi walipata hasara, kupoteza mali na mtoto wao, wale ambao hatujaoa kweli ndugu zangu, tukifikiri hilo hatutaoa tena."

Haya ni mashairi ya wimbo uitwao 'Kifo cha Mukabi', ambao ulitungwa na kuimbwa na mwanamuziki John Mwale kutoka nchini Kenya.

Alitunga wimbo huo ulio kwenye mtindo wa 'twist' mwanzoni tu mwa mwaka 1960, kufuatia kifo cha kiunyama cha mwanamuziki mwenzake, George Mukabi.

Mukabi alikuwa mwanamuziki maarufu, siyo nchini Kenya tu alikozaliwa, hata nchini Tanzania ambapo alikuwa na mashabiki lukuki kutokana na nyimbo zake kali kugusa watu wengi wakati huo.

Kifo chake sio tu kwamba kilileta pigo kwa mashabiki wa muziki Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, lakini kilileta taharuki kubwa kutokana na mazingira yenyewe.

Utakumbuka kuwa wakati huo teknolojia haikuwa kubwa sana miaka ya 1950 hadi 1970, na nyimbo hizo zilipatikana kwenye santuri au sahani ambazo zilijulikana kama GV.

Ni miaka ambayo nyimbo za wanamuziki hao zilipigwa kwa magitaa baridi, yaani yasiyotumia umeme, maarufu kama 'magalatoni' zikihamishwa mapigo ya chupa, ngoma, au manyanga, mbao, au bati ili kunogesha muziki. Hakukuwa na nyombo vingi.

Pamoja na hayo wanamuziki wa enzi hizo walikuwa mahiri sana, kwani pamoja na uduni kwa vyombo, waliweza kurekodi nyimbo mbalimbali zilizokuwa kwenye santuri ambazo zilivuma na kupendwa sana Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Congo ya Kibelgiji, sasa Jamhuri ya Kidemokrasi cha Congo, kulikuwa na wanamuziki waliopendwa mno nchini wao na nyimbo zao kama Jean-Bosco Mwenda wa Bayeke, Edward Masengo, Losta Abelo, Uganda mwanamuziki aliyekuwa maarufu Bongo ni Charles Sonko na dada yake Frida Sonko, nchini Zambia kulikuwa na Nashil Pitchen na Peter Tsosi, huku Kenya kulikuwa na kina Daudi Kabaka, John Zenze, John Mwale, Fadhili William, akiwemo pia Mukabi.

Mkenya huyo alizaliwa 1930 na kuuawa mwaka 1963 akiwa bado kijana tu wa miaka 33 na tayari alikuwa ameshaanza kupata mafanikio kwenye karia yake ya muziki.

Ulivuka mipaka ya Kenya na kuwa na mashabiki wengi nchini Tanzania, huku nyimbo zake maarufu ambazo zimeendelea kupendwa hadi leo hii ni 'Sengula Nakupenda', 'Kweli Ndugu' na 'Mtoto Si Nguo'.



Mwanamuziki maarufu nchini Kenya miaka ya 1960, George Mukabi, ambaye aliuawa kinyama katika tukio la kushangaza ambalo limebaki kuwa ni simulizi hadi leo hii.

Kabla ya kuelezea kisa kizima kilichosababisha kukatishwa nyota, hebu tuangalie mashairi ya nyimbo zake tatu ambazo ndizo zilizokuwa ziki

"Sengula ninakupenda, si nikuwa napenda, Sengula we kweli Sengula wangu, si nilikuwa nakupenda?

Ni vizuri tupendane, nyumba ikawa na heshima, Sengula we kweli Sengula wangu si nilikuwa nakupenda.

Ninachoka na mambo yako, Sengula we kweli Sengula wangu si nilikuwa nakupenda."

Huu ndiyo wimbo bora zaidi na ulikuwa ukimtambulisha mwanamuziki huyo na kumpatia sifa na aliuza nakala nyingi mno.

"Mtoto si nguo utaomba mtu, ukikosa mtu baba, ukikosa wako utalia sana baba. George mwamba sina wangu mie, nakosa wangu ee ninalia sana baba." Nao ulipendwa sana nchini Tanzania na kufuatia ule wa 'Kweli Ndugu"

"Kweli wangu sikilizeni niwambieni, kwa kuoa nilikooa bibi mmoja mrembo, sasa kaleta hasara kuvunjavunja vikombe, kuvunja vunja sahani.

Na wandugu wangu wote walikataa, walisema afunge aende, hatutaki hasara, avunjavunja vikombe, avunjavunja sahani."

Alitunga na kuimba nyimbo nyingi sana kwa muda mfupi tu wa maisha yake, lakinbi hizo tatu zilitia fora sana hasa nchini Tanzania.

Kifo chake kilikuwa na uvumi mwingi, ikiwemo kuwa alioa mke, baada ya siku chache mke akakimbia akarudi kwao, akaamua kumfuata na huko akauawa na hawara wa mkewe.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi nchini Kenya baada ya kufanya uchunguzi wake liligundua kuwa kisa cha kifo chake hiki.

Baada ya kupiga muziki wake kwenye Jiji la Nairobi alirejea kwao Kakamega na kufikia nyumbani kwa mke mdogo. Akaweka gita lake na kumwambia anakwenda kulala kwa mke mkubwa. Mke mdogo wivu ukamshika, pia akadhani kuwa pesa zote alizopata kwenye muziki atakwenda kupewa mke mkubwa.

Wakati yupo nje anaondoka, mke mdogo kwa hasira akaamua kuchukua gitaa la mumewe na kulivunja. Ikumbukwe lilikuwa ni gitaa jipya kabisa la kisasa wakati huo ambalo alipewa na rafiki yake raia wa Uingereza. Aliposikia kama kuna sauti za kuvunja kitu, akarejea na kukuta gita lake linevunjwa. Mke akaamua kukimbilia kwao . Mukabi kwa hasira na yeye akamfuata. Mke alipofika kwao akakimbilia moja kwa moja chumbani kwa baba yake. Mukabi akaingia humo humo. Baba mkwe alikuwa nje na aliona timbwili lile. Bila kufikiria akaanza kupiga yowe kuita majirani wamsaidie. Wanakijiji wao walipofika hawakuuliza, wakaanza kumpiga Mubaki kwa mapanga, mawe, rungu shoka na kila aina ya silaha za jadi. Binfasi nina wasiwasi labda aliita kelele za mwizi. Ilikuwa ni usiku.

Kwa kujaribu kujiokoa akakimbia na kuvuka mto Yala, lakini hakuweza kufika mbali, aliishiwa nguvu akaanguka na kuzimia.

Bado wanakijiji wao wa Bososo waliendelea kumkimbiza na walipomkuta wakamalizia kwa mawe, kabla kumkatakata vipande kama nyama. Sehemu ya mwili wake wakaipakia kwenye mkokoteni na kuipeleka kwenye hospitali ya Kakamega.

Lilikuwa ni tukio la kusikitisha sana. Mwanamuziki mmoja wa Kenya naye alitunga wimbo wa kuwashutumu wanajiji hao akaimba. "Watu wa Busoso walimkata George kama mti."

**Tuma meseji 0716 350534**




Hili ni kaburi la Mukabi lililipo Kakamega nchini Kenya, anayeonekana kukaa hapo na mtoto wake, Johnstone Mukabi ambaye amerithi kazi ya baba yake ya muziki.

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yapinga mauaji ya Haniyeh

**NEWYORK,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, amesema kuwa mauaji ya kiongozi wa Hamas Ismail Haniyeh, hayasaidii kuleta amani Ukanda wa Gaza.

Biden alisema tukio hilo linarudisha nyuma mazungumzo kuhusu uwezekano wa kusitisha mapigano yanayoendelea Gaza.

Haniyeh aliuawa siku moja katika ziara yake katika mji mkuu wa Tehran nchini Iran.

Iran na washirika wake wameilaumu Israel kuhusika katika mahojiano hayo, ingawa Israel bado haijatoa maoni yoyote kuhusu kifo chake.

Haniyeh alikuwa kiongozi mkuu wa Hamas na alihusika sana katika mazungumzo ya kusitisha mapigano na kuwaachilia mateka kutoka kituo chake nchini Qatar.

Rais Biden alisema ana hofu kuhusu kuongezeka kwa mvutano katika Mashariki ya Kati.

"Tuna msingi wa kusitisha mapigano. Yeye (Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu) anapaswa kuendelea nao na Hamas wanapaswa kuendelea nao sasa." Alisema Rais Biden.

Israel na Hamas hivi majuzi walianza tena mazungumzo yasiyo ya moja kwa moja ili kujaribu kufikia usitishaji wa vita, ingawa kumekuwa na maelezo yanayokinzana kuhusu mafanikio ya mazungumzo hayo.

Mwishoni mwa mwezi Mei, Rais Biden alieleza kile alichosema kuwa ni masharti ya pendekezo la Israeli la kusitisha mapigano. Mapema wiki hii, Israel na Hamas zilishutumu kila mmoja kwa kukwamisha maendeleo ya mazungumzo.

Wakati huo huo, mazishi ya aliyekuwa kiongozi Mkuu wa kisiasa ya Hamas, Ismail Haniyeh,yamefanyika nchini Qatar jana. Jeneza lilobeba mwili wa Haniyeh, ambaye aliuawa pamoja na mlinzi wake wake wa kibinafsi, liliwasili Doha katika makazi yake katika mji mkuu wa Qatar, kabla ya kuelekea msikitini kwa ajili ya swala ya mazishi.

Kabla ya kuwasili nchini Qatar, maelfu ya watu katika mji mkuu wa Iran, walishiriki kuaga mwili wa Haniyeh.

Kiongozi Mkuu wa Iran, Ayatullah Ali Khamenei, aliwaongoza waumini katika swala ya mazishi iliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Tehran. Nchi ya Qatar imekuwa makazi ya kiongozi huyo na wanachama wengine wa kisiasa ya Hamas.

**BBC**



Vikosi vya usalama vya Nigeria vikirusha mabomu ya kutoa machozi kuwatawanya waandamanaji wanaopinga serikali kwa kupanda gharama za maisha jana. **PICHA: REUTERS**

# Russia yabadilishana wafungwa na Marekani

**WASHINGTON,** MAREKANI

ZOEZI kubwa la kubadilishana wafungwa tangu kumalizika vita baridi limefanyika kati ya Russia na nchi za Ulaya na Marekani.

Marekani ilithibitisha kuwa wafungwa 24 waliachiliwa huru katika mbadilishano hayo.

Ikulu ya Marekani ilisema wafungwa 16 walikuwa wameachiliwa na walirejea Ulaya na Marekani.

Miongoni mwa wafungwa hao ni mwandishi wa jarida la Wall Street Journal, Evan Gershkovich.

Kwa upande wake, wafungwa wanane wa Russia waliachiliwa huru kutoka magereza nchini Marekani, Norway, Ujerumani, Poland na Slovenia, wakiwemo watu wanaotuhumiwa kwa shughuli za kijasusi.

Watoto wa wafungwa wawili pia walirudishwa Russia.

Mabadilishano hayo yalifanyika Alhamisi kwenye barabara ya kurukia ndege katika uwanja wa Ankara nchini Uturuki.

Rais Joe Biden alithibitisha kuwa mwanajeshi mkongwe wa Wanamaji wa Marekani, Paul Whelan, mwandishi wa habari mwenye asili ya Russia na Marekani Alsu Kurmasheva na mwanaharakati wa Russia mwenye asili ya Uingereza Vladimir Kara-Murza walirejea nchini Marekani.

Makubaliano hayo yalifanyika baada ya mazungumzo ya zaidi ya miezi 18 na yalionekana kujumuisha matakwa ya Russia kutaka Vadim Krasikov arejeshwe nyumbani.

Alikuwa akitumikia kifungo cha maisha jela nchini Ujerumani kwa kutekeleza mauaji katika bustani ya Berlin.

Maafisa wakuu wa utawala wa Marekani walimtaja kama mtu mbaya na kusema alikuwa muhimu zaidi ambaye Russia ilitaka arejeshwe.

**BBC**

# Watu 13 wauawa nchini Nigeria

**ABUJA,** NIGERIA

WATU 13 wamefariki dunia wakati wa maandamano ya kupinga serikali na kupanda kwa gharama ya maisha nchini Nigeria.

Shirika la kutetea haki za binadamu la Amnesty International, lilisema polisi walitumia kuvu kubwa kuwadhibiti waandamanaji na kusababisha vifo vya watu hao ambao walikuwa wakiandamana kwa amani.

Ilisema katika taarifa yake katika mtandao wa X, kuwa watu sita waliuawa katika mji wa Suleja, karibu na mji mkuu Abuja, wanne Maiduguri na watatu waliuawa huko Kadun.

"Ushahidi wetu, katika hatua hii, unaonyesha kwamba pale palipokuwa na vifo, askari wa usalama walitumia mbinu za makusudi kuua wakati wakikabiliana na mikusanyiko ya watu wanaokemea njaa na umaskini mkubwa," limeandika shirika hilo.

Awali, Mkuu wa Polisi nchini humo, alikanusha shutuma kwamba polisi waliwashambulia waandamanaji.

Katika taarifa iliyochapishwa kwenye mtandao wa X, mkuu wa polisi Kayode Egbetokun alisema ameweka vitengo vyote kwenye tahadhari kujibu vitisho kwa usalama na utulivu wa umma.

Vikosi vya usalama jana vilifyatua mabomu ya kutoa machozi kwa waandamanaji waliokuwa wakishiriki katika siku ya pili ya maandamano hayo.

**RFI**

# Mazungumzo kutafuta amani DRC yaendelea

**LUANDA,** ANGOLA

Rais wa Angola, Joao Lourenco, amekuwa na mazungumzo kwa njia ya simu na marais Paul Kagame wa Rwanda na Felix Tshisekedi, wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, katika kutafuta makubaliano ya usitishaji mapigano.

Hivi karibuni Rais wa Angola na DRC, walikutana kuzungumzia suala hilo la usitishaji mapigano.

Aidha makubaliano hayo yamepokelewa vizuri na viongozi wengine wa nchi za kikanda, ambao wanaamini kuwa ikiwa yatatekelezwa kikamilifu kuanzia Agosti 4, mwaka huu.

Mazungumzo hayo yanatokana na mchakato wa kutafuta Amani yaliyofanyika nchini Kenya kuonekana kukwama. Uamuzi wa viongozi hao wa kuridhia kusitisha mapigano unatoa nafasi ya mazungumzo zaidi kuelekea suluhu ya kudumu.

Hayo yanajiri wakati wataalamu wa masuala ya usalama kutoka Angola, Rwanda na DRC wanatarajiwa kukutana Agosti 7, kutathmini utekelezwaji wa makubaliano hayo.

**RFI**



# Kunahitajika usimamizi madhubuti kwenye ghala la pembe za ndovu

**Na Mwandishi Wetu**

FEBRUARI 28, mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, mkoani Mara, kwa tuhuma za kushiriki wizi wa fedha za umma zaidi ya Sh. milioni 213.

Akiwa ziarani wilayani Serengeti siku hiyo, Waziri Mkuu Majaliwa aliwataja wahusika wa wizi huo, ambao alisema wanashirikiana na watumishi wengine watatu kutoka Kitengo cha Treasury Single Account (TSA) cha Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Majaliwa aliutaja ni mtandao wa wizi wa fedha za umma ambao si tu umebainika wilayani Serengeti, bali pia uko katika maeneo mengine nchini, ikiwamo mkoani Kigoma ambako nako alishabaini shida hiyo katika ziara zake zilizotangulia.

Kwa mujibu wa Majaliwa, wahusika wa wizi huo wa fedha za umma, wanafikia hadi kusafirisha fedha hizo kwa mabasi wakiziweka katika mabegi ya nguo.

Wakati umma ukisubiri kuona hatua zinazochukuliwa dhidi ya watumishi hao, wakiwamo wanaotoka maeneo nyeti - Ofisi ya Rais, kuna dosari nyingine katika usimamizi wa ghala la pembe za ndovu nchini.

Kulikoni? Katika ripori yake ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ameangazia suala hilo, akipendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia pembe za ndovu nchini.

CAG pia anapendekeza wizara iandae mfumo madhubuti wa taarifa zote zinazohusiana na pembe za ndovu, ukiwamo mpango mkakati wa taarifa za upotevu kutokana na matukio yasiyotarajiwa kama vile moto.

Shida ni nini? CAG anasema kuwa wakati wa ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Maliasili na Utalii, amebaini kuwa Mei 16, 2022, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, aliunda timu ya uhakiki wa mali ambayo ilijumuisha wajumbe kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori nchini (TAWA), DW, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Anasema timu hiyo iliundwa kwa lengo la kuanzisha mchakato wa kuhesabu na kupima akiba ya nyara katika ghala la Dar es Salaam. CAG anasema alibaini pamoja na mengine, kutopatikana taarifa sahihi za pembe za ndovu zilizohifadhiwa kwa ajili ya kufanya tathmini na kuzipima upya pembe hizo.

Anasema kuwa pia alibaini hali isiyoridhisha ya pembe zote zilizohifadhiwa kiasi cha kusababisha kuharibika ubora na hadhi yake.

CAG pia anasema alibaini shida nyingine ya kushindwa kuhusisha rejista juu ya hali na thamani ya pembe za ndovu, programu iliyotumika kurekodi na kusajili akiba ya pembe za ndovu na nyara zingine kutounganishwa na seva kuu ya programu ya wizara kwa sababu programu hiyo ilikuwa imepitwa na wakati.

> **"Kwa maoni yangu, ukosefu wa udhibiti sahihi wa pembe za ndovu unaweza kusababisha upotevu wa taarifa zinazohusiana na pembe hizo," anahadharisha.**

CAG anasema katika ripoti yake hiyo kuwa, baadhi ya pembe za ndovu zilikosa taarifa zake za maandishi huku zingine zikiwa na taarifa zisizosomeka kutokana na ubovu wa paa la kuhifadhia, jambo linalosababisha kuvuja kwa paa hilo. Anaongeza kuwa amebaini pia zana za kuwekea alama zilizotumiwa kurekodi taarifa kuhusu pembe za ndovu, ziliandikwa kwa wino unaoweza kufutika, na kuzifanya ziweze kufutika kwa urahisi.

CAG anasema ghala la kuhifadhia nyara hizo lilikuwa katika hali mbaya kutokana na kuwa na nafasi ndogo, paa kuvuja, hewa chafu, mazingira machafu, umeme usio imara, ukosefu wa kamera na vifaa vya kuzima moto.

CAG anasema kuwa mbali na hayo, pia amebaini kuwa mwaka 2013, kulikuwa na tukio la moto katika ghala la pembe za ndovu ambalo lilisababisha kupotea kwa taarifa muhimu zinazohusiana na pembe za ndovu zilizohifadhiwa.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anasema ni jambo la kushangaza kuwa hakuna uchunguzi uliofanyika ili kubaini chanzo cha moto huo na madhara yake hadi wakati wa ukaguzi wake.

"Kwa maoni yangu, ukosefu wa udhibiti sahihi wa pembe za ndovu unaweza kusababisha upotevu wa taarifa zinazohusiana na pembe hizo," anahadharisha.

CAG anasema taarifa kuhusu pembe za ndovu ni muhimu katika kesi za kisheria dhidi ya ujangili na juhudi zingine zinazolenga kudhibiti vitendo vya ujangili.

Vilevile, CAG anabainisha kuwa menejimenti ya Wizara ya Maliasili na Utalii imethibitisha kuwapo upungufu huo huku ikiahidi kufanya uhakiki wa nyara kila baada ya miaka mitatu hadi minne, kulingana upatikanaji wa rasilimali.

Kimsingi, yaliyobainishwa na CAG yanapaswa kufanyiwa kazi ikizingatiwa nchi bado inakabiliwa na changamoto ya ujangili hasa wa tembo na faru ambao kuna kipindi waliripotiwa kuwa hatarini kutoweka nchini.

Sekta ya Utalii inachangia takriban robo ya fedha zote za kigeni nchini, ikiajiri watu 600,000 ofisini na wengine zaidi ya milioni mbili iliowapa ajira zisizo za moja kwa moja.

Ujangili ukifumbiwa macho, bila kuwapo ufanganyifu katika maghala ya kuhifadhi nyara za serikali, utahatarisha ya uhai wa wanyama wanaolengwa zaidi na majangili, hasa ndovu na faru, hivyo kuuweka rehani pia uchumi wa nchi. Sekta ya Utalii ambayo mchango mkubwa katika Pato ya Taifa.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.

Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana akiwa anakimbia, au anakwenda jogging.

Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani ilionekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.

Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli pia wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-24

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Aliwalipa ujira wenu?" Willy akauliza "Ndiyo mimi alinilipa changu na mimi ndiyo niliowalipa hao wengine." "Okay, basi usimwambie chochote kile hasa nilipondoka hapa. Kitendo cha kumwambia kitakufanya wewe uwe kwenye hatari ya kuuawa hata kama ni rafiki yako." Afande Willy alionya "Sawa afande" Akaitika Kalisa.

Kwa upande wake Kalisa Mohamed alikubaliana na afande Willy. Alimfahamu vyema rafiki yake. Alijua kabisa kama suala lenyewe litahusisha kumshushia heshima na kumfedehesha mbele ya jamii, basi asingekuwa na msamaha. Hakuthubutu kumwambia.

Willy baada ya kulipata jina lile hakushangaa sana, ila mtu yoyote wa kawaida angeshangaa na mwingine asingekubali kabisa. Lakini kwa sababu yeye ni askari ambaye mara nyingi ameshaona watu ambao wanaheshimika kwenye jamii baadhi yao nyuma ya pazia si watu wazuri, na wamekuwa wakitumia nguvu ya pesa kuficha maovu yao.

Kwa jinsi sakata lilivyo, afande Willy, aliona yupo mwishoni mwa kitendawili kizima cha nani alimuua Mariam? Nani aliwahonga madaktari kupindisha uchunguzi? Nani aliyemsingizia mpenzi wa Mariamu, Kamal kuwa muuaji? Kwa nini aliwarubuni askari polisi kuamini kuwa Kamal ndiye muuaji baada ya uchunguzi wa pili kufanyika? Kile alichokuwa akikifikiria tangu mwanzo sasa anaona kimeanza kutimia.

Hata hivyo alitaka kujidhihirisha kama ni kweli. "Inawezekana naye akawa kama Kalisa. Labda kuna mtu mwigine juu yake." Akajiambia. Uchunguzi wake huo hakuupeleka ofisini, bali watu wake wa kuwasiliana nao ni wawili tu. Kama dokta Shija na Kamal, mpenzi wa marehemu Mariamu ambaye anatafutwa kwa udi na uvumba kwa tuhuma za kumuua mpenzi wake.

*********************************

Simu ya Kamal iliita ikiwa mkononi mwake. Hakuwa anapigiwa na watu wengi, hivyo kwa muda huo alikuwa na Dokta Shija tu. Na kweli ilikuwa hivyo. "Naomba uje ofisini kwangu Ilala tafadhali, nina maagizo yako kutoka kwa Willy." "Sawa dokta." Kamal hakuwa tena na wasiwasi na dokta. Ni mtu ambaye kwa kiasi kikubwa amemsaidia hadi pale alipofikia. Pamoja na kujificha, lakini kazi aliyokuwa akiifanya ya kumsaka muuaji na mpenzi wake ilirahisishwa zaidi na dokta huyo. Alikipongeza kitendo chake cha kujifanya anaumwa na kwenda kwenye zahanati ya daktari huyo, ambayo ndiyo ilimfanya kukutana naye. Japo aliondoka kwa ajili ya kile alichokiita usalama wake, lakini baadaye aligundua ni mtu mwenye nia safi ya kumsaidia. Kujiingiza kwenye janga lile, tena akiwa amemshirikisha mdogo wake, ilikuwa ni zaidi ya urafiki au undugu.



"Nashukuru sana kukufahamu, maana kila siku tunaongea kwenye simu tu." Willy alimpa mkono Kamal huku akimkaribisha nyumbani kwake.

Hakutaka hata kupanda gari wala bodaboda, aliambaaambaa na njia za mkato hadi akafika kwenye zahanati ya dokta Shija iliyopo Ilala.

Baada ya kusalimia akakaakaa. Alipomaliza kumpa majibu ya vipimo mgonjwa mmoja, alifunga mlango na kumwambia. "Bwana jamaa amefanya ile kazi, amekamata watu wawili kwa nyakati tofauti, nao walimtaja mtu mmoja aliyewapa hiyo kazi. Akaenda kwa huyo aliyewapa kazi, naye akamwambia mtu mmoja ambaye ni mkubwa na maarufu hapa nchini. Sasa anakuhitaji wewe ili akupe hilo jina kama unamfahamu. Unaweza ukawa unamfahamu kwa ajili ya ukubwa na umaarufu wake, je uliwahi kukutana naye au kukorofishana naye huko nyuma? Na wewe ndiyo unaweza kumpa ukweli kama inawezekana akawa ndiyo mhusika!" "Vizuri twende zetu." Dokta Shija alitoka na kumwita kijana mmoja ambaye alionekana ni daktari mwanafunzi. Akamuachia maelekezo juu ya vitu kadhaa na kumuashiria Kamal waondoke.

Walipanda kwenye gari na safari ilikuwa ni kuelekea Mtoni anapokaa mdogo wake, afande Willy.

*******************************

"Nashukuru sana kukufahamu, maana kila siku tunaongea kwenye simu tu." Willy alimpa mkono Kamal huku akimkaribisha nyumbani kwake.

Kwa jinsi ilivyoona kwenye nyumba hiyo ilionekana kabisa afande Willy hakuwa na mke.

"Ahsante sana afande Willy, nashukuru sana kwa msaada wako. Kusema kweli nilikuwa najaribu kumsaka mtu aliyefanya mauaji ya Mariamu, lakini ilikuwa ngumu, lakini tangu umeamua kunisaidia, nadhani ni kama tunapiga hatua moja kila siku kwenda mbele." Alijibu Kamal huku akikaa kwenye siti ambayo alikaribishwa. Kamal alikaa jirani na afande Willy, huku dokta Shija ambaye ndiye aliyeunganisha akakaa pembeni kidogo, ingawa alikuwa ni mmoja wa watu muhimu kwenye maongezi.

Hata hivyo ilieleweka kabisa kuwa Kamal na Willy ndiyo walikuwa na maongezi maalum kwani mmoja ni mhusika na mwingine mtekelezaji aliyejitolea kumsaidia kwa vitendo.

Walianza kwa kutaniana, baadaye kila mmoja kueleza historia ya maisha yake, na hasa iliyovutia zaidi ilikuwa ya Kamal, ambaye alisimulia jinsi walivyokutana na mpenzi wake katika basi Mkoani Morogoro, walivyovurugana hadi kuelewana kwa namna ya kushangaza na baadaye kuwa wapenzi, na mwishowe kuuawa.

Alihadithia jinsi vitisho vilivyoanza na hatimaye kuuawa, na yaliyofuatia sasa wote walikuwa wanayafahamu.

Historia hiyo ilimshangaza sana Dokta Shija ambaye ilionekana kumgusa zaidi, na akamtazama kwa huruma Kamal. Ingawa walikuwa wameshazoena na kufahamu kila kitu hadi alipobambikiwa tuhuma, lakini bado alikuwa hajawahi kufahamu mwanzo wa uhusiano wa kijana huyo na mpenzi wake na jinsi penzi lao lilivyowakolea, jinsi walivyopendana mpaka vidudu mtu kuingia kati na kulitengenisha.

"Nimekuita hapa ili nikupe mrejesho wa kile ambacho tumekifanyia kazi mimi na wewe." Afande Willy alianza kile ambacho kimewaleta pale. "Nakumbuka kwanza nilihitaji namba za simu ambazo zilitumika kukutumia meseji za vitisho wewe na mpenzi wako ambazo uliniambia hata ukijifanya kama unataka kuwatumia pesa, haitoi majina ya watu, nikwambia namba haipo." "Ni kweli afande."

"Niliifanyia kazi na nikakwambia namba hizo nne, zilisajiliwa na wakala Shida Mrosso pale Tabata, ukaenda kuzifanyia kazi." "Ndiyo." "Unaniletea majina ya Uledi Mwinyimvua alisajili laini mbili za makampuni tofauti na Abbas Abdallah naye alisajili mbili pia." "Ni kweli afande." "Sasa uliponipa nilendelea kufanyia kazi suala hili. Kama nilivyokwambia nitaifanya bila kibali kutoka Jeshi la Polisi, ila kwa ajili ya kukusaidia kama raia mwema, rafiki wa kaka yangu, na pia ikibainika hiki kitu kinaweza kunipa sifa kubwa, ingawa nimejiingiza kwenye hatari kutoka kwa wenzangu ambao ni wala rushwa. Lakini sijali hilo. Nilikwenda kuwakamata hao wote wawili kila mmoja kwa wakati wake. Wote wakaniambia wametumwa na mtu mmoja anayeitwa Kalisa Mohamed." Akanyamaza na kumtazama Kamal alivyokuwa anashangaa. "Unamfahamu?" "Hapana simfahamu. Labda nikimuona kwa macho." "Okay, kama askari nikambana, akakubali kuwa ni kweli aliwatuma watu wale waende wakasajili laini hizo, lakini na yeye alitumwa na rafiki yake mkubwa, anaitwa Boniphace Materu." Alipotamka jina lile Kamal alishtuka na macho yalimtoka pima, kiasi cha kuwashangaza na kuwashtua afande Willy na Dokta Shija. Ilionekana kabisa moja kwa moja anamfahamu sana mtu huyo.

*Itaendelea Jumamosi*

# Wananchi waitwa tamasha la ZIFF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WANANCHI wa Zanzibar wametakiwa kujivunia na kujitokeza kwa wingi kuangalia filamu zinazooneshwa katika tamasha la Kimataifa la filamu „ZIFF " linaloendelea hapa Zanzibar.

Tamasha hilo la 27 limeanza juzi, Agosti Mosi na linatarajiwa kufikia tamati kesho.

Akizungumza na wanahabari jana, Mkurugenzi Mtendaji wa tamasha hilo la Kimataifa, Khatibu Madudu, alisema Tanzania na Zanzibar imepata bahati ya kuoneshwa filamu ambazo hazijawahi kuoneshwa sehemu yoyote.

Alisema Wananchi watumie fursa hiyo katika tamasha hilo kubwa kwa kufatilia filamu mbalimbali ambazo zinaonyeshwa ili kujifunza mambo yanayoendelea kupitia filamu hizo.

Alisema tamasha hilo kubwa linatoa fursa mbalimbali linapofanyika Zanzibar ikiwa pamoja na kuitangaza nchi, lakini pia watu kufanya biashara kupitia bidhaa za wajariamali wanazouza kwa wageni ambao wanafika hapa nchini kwa ajili ya kufuatilia tamasha hilo.

**"Tunawapongeza sana wananchi kwa mua mko wao mkubwa ka tika kulipokea tama sha hili, tulianza jana kwa shughuli mbalim bali katika maeneo ya hapa Ngome Kongwe lakini pia hata nje ya mji wa Zanzibar, hivyo tunawaomba waendelee kujitokeza kwa wingi," alisema Madudu.**

Aidha alisema kuwa mpaka kufikia sasa wameanza kupata mrejesho mzuri kwa filamu ambazo zimeonyeshwa siku ya ufunguzi kutokana na kubeba maudhui mazuri yanayoendana na uhalisia wa maisha ya sasa.

Katika tamasha hilo la Kimataifa la Filamu kwa mwaka huu jumla ya filamu 70 zitaonyeshwa kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

# TANZANIA YAPANIA KUFANYA VIZURI KRIKETI AFRIKA

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa timu ya taifa ya vijana chini ya miaka 19 ya mchezo wa kriketi, Salum Jumbe, amesema wamejiandaa vizuri kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye ardhi ya nyumbani katika mashindano ya mchezo huo wa divisheni ya pili Afrika.

Michezo hiyo ilianza kutimua vumbi jana kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es salaam ambapo nchi nane za Afrika zinashiriki.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika mkutano wa kuzitambulisha nchi shiriki katika mashindano hayo, Jumbe alisema kutokufanya vizuri katika mashindano ya mwaka jana, kwao wanachukulia kama chachu ya kuhakikisha wanafanya vizuri mwaka huu.

„Mwaka jana hatukufanya vizuri na kujikuta tukishuka daraja, mwaka huu mashindano haya yanafanyika hapa nyumbani, tumejipanga na tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunafanya vizuri na kupanda daraja," alisema Jumbe.

Aidha, nahodha wa timu hiyo, Lakshi Bakrania, alisema waliumia sana mwaka jana kwa kutofuzu licha ya kujituma lakini mwaka huu wamejiandaa kuhakikisha wanaipeperusha vyema bendera ya Tanzania katia mashindano hayo.

„Mwaka huu tuna timu mpya na malengo mapya, tutapambana kuhakikisha tunafanya vizuri, haitapendeza kushindwa tukiwa kwenye ardhi ya n yumbani," alisema Bakrania.

Kwa upande wake, mratibu wa mashindano hayo yanayoandaliwa Baraza la Kimataifa la Mchezo huo (ICC), ATif Salim, alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi za Nigeria, Ghana, Sierra Leone, Malawi, Msumbiji, Botswana, Rwanda na wenyeji Tanzania.

„nchi hizi zitagawanywa kwenye makundi mawili, na timu mbili katika kila kundi zitasonga mbele kucheza fainali na moja kwa moja zitakuwa zimepanda daraja, timu moja tutaipata kwa kuchukua timu zilzioshika nafasi ya tatu kila kundi watacheza mchezo mmoja kusaka nafasi ya tatu ambayo ataungana na timu nne kuingia divisheni ya kwanza," alisema Salim.




Nahodha wa timu ya taifa ya mchezo wa Kriketi ya Tanzania, Laksh Bakrania (katikati), akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu Mashindano ya ICC Afrika Divisheni ya npili yaliyoanza jana kwenye viwanja vya Gymkhana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kushoto ni kocha wa timu hiyo, Salum Jumbe, kulia ni Mratibu wa mashindano hayo, Atif Salim. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Queens yaanza kambi ya Ligi ya Mabingwa Afrika

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Simba Queens, wameanza rasmi mazoezi na kambi ya kujiandaa na michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kanda ya CECAFA inayotarajiwa kuanza Agosti 17 nchini Ethiopia.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, amesema kikosi chake chote kimeanza mazoezi wakiwemo wachezaji wapya ambao wamesajiliwa kutoka klabu mbalimbali lengo likiwa ni moja tu kwenda kufanya vyema na hatimaye kutwaa ubingwa ili kurudisha heshima iliyopotea msimu uliopita.

„Nimeona ari na morali ya wachezaji iko juu, wanataka kwenda kushindana, lakini kikubwa kinachotupa matumaini ni imani ni wenyewe wanajua huko wanakwenda sokoni, lazima mtu atayarishe bidhaa yake nzuri ili ikauzike.

Vijana wanaelewa Simba wanataka nini, nchi inataka nini na wao wanahitaji nini kwenye mashindano hayo, kifupi wana utayari wa kwenda kushindana," alisema Mgunda ambaye juzi alitwaa tuzo ya kocha bora kwa timu za wanawake.

Naye mmoja wa wachezaji tegemeo kwenye timu hiyo, Vivian Corazone, amesema msimu huu wanataka kufanya kama walivyofanya mwaka juzi, walipofika hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa katika fainali zilizochezwa nchini Morocco.

„Maandalizi yanaendelea, makocha wanafanya kazi yao wakimaliza kazi inabaki kwetu, tunajua msimu uliopita JKT Queens walikuwa mabingwa wa CECAFA, wakapata tiketi ya kwenda fainali ya Ligi ya Mabingwa, na sisi lengo letu ni moja kwenda kuchukua kombe na kutinga fainali kama msimu wa mwaka juzi ambao tulifika nusu fainali," alisema kiungo huyo raia wa Kenya.

Tayari Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), limetoa ratiba ya ligi hiyo, ambayo itaanzia kwa ngazi ya kanda, ambapo Ukanda wa CECAFA, Simba Queen ipo Kundi B ikiwa na timu za PVP Buyenzi ya Burundi, Kawempe Muslim Ladies ya Uganda na FAD ya Djibouti.

Simba Queens inatarajiwa kucheza mchezo wake wa kwanza Agosti 18 itakapoumana na FAD.

Bingwa wa michuano hiyo atakuwa amepata tiketi ya kucheza fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika, akiungana na mabingwa wa kanda nyingine.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**LUKAKU KUMPISHA OSIMHEN**
CHELSEA inajadili mpango wa mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, kujiunga na Napoli, huku mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, akitarajiwa kuhamia klabu hiyo kwa mkopo. ***(Athletic)***

**GROSS KUTIMKIA DORTMUND**
KLABU ya Brighton imekubali mkataba wa pauni milioni 5.9 kumruhusu kiungo wa kati wa Ujerumani, Pascal Gross mwenye umri wa miaka 33, kujiunga na Borussia Dortmund. ***(Guardian)***

**RABIOT MBIONI KUTUA UNITED**
KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, anakaribia kusaini Manchester United baada ya kuondoka Juventus mwishoni mwa mkataba wake. ***(Mail)***

**SETFORD ATAKIWA ARSENAL**
ARSENAL inajiandaa kumsajili mlinda mlango wa Uingereza, Tommy Setford mwenye umri wa miaka 18 kutoka Ajax ua Uholanzi. ***(Evening Standard)***

**LINDSTROM KWA MKOPO EVERTON**
KIUNGO wa kati wa Denmark, Jesper Lindstrom mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kucheza kwa mkopo wa msimu mzima pale Everton kutoka Napoli. ***(CalcioMercato)***

**GOMEZ AWINDWA BRIGHTON**
KLABU ya Brighton imefanya mazungumzo na Inter Miami kuhusu mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Paraguay, Diego Gomez mwenye umri wa miaka 21.***(Sky Sports)***

**HARRIS AWANIWA BIRMINGHAM**
KLABU ya Birmingham City imeelekeza macho yao kwa kiungo wa Fulham na Wales, Luke Harris mwenye umri wa miaka 19. ***(Football Insider)***


**KANTE KUTUA WEST HAM**
KLABU ya West Ham imefikia makubaliano ya mdomo ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 33 kutoka Al Ittihad. ***(The Athletic)***

**ASTON VILLA KUMUUZA DIGNE**
ASTON Villa inajiandaa kumuuza mlinzi wa Ufaransa, Lucas Digne mwenye umri wa miaka 31. ***(Football Insider)***

**UGARTE, UNITED MAMBO SAFI**
KIUNGO wa kati wa Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 23, amekubaliana maslahi binafsi na Manchester United, ambao wanaendelea kufanya mazungumzo na Paris St-Germain. ***(Fabrizio Romano)***

**MCTOMINAY APANGIWA BEI**
MANCHESTER United imeweka bei ya pauni milioni 30 kwa kiungo wa kati wa Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MIKEL ARTETA: ARSENAL INAHITAJI KUIMARIKA ZAIDI

Kocha huyo ametoa tathmini yake baada ya kumaliza ziara kwa kipigo cha....

**LOS ANGELES, Marekani**

MIKEL Arteta ametathmini kiwango cha Arsenal kabla ya msimu mpya kufika baada ya kumaliza ziara yake ya Marekani kwa kupokea kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Liverpool.

Washikabunduki hao ambao waliwashinda Bournemouth na Manchester United kabla ya kukabiliana na Wekundu hao kwenye Uwanja wa Lincoln, hawakuweza kufurukuta mbele ya vijana wa Arne Slot wakifungwa mabao mawili kabla ya kipindi cha mapumziko huko Philadelphia.

Akizungumza na vyombo vya habari baada ya kupoteza, Arteta alikiri kwamba timu yake lazima ibadilike na kuimarika ikiwa wanataka kushindana katika msimu ujao wa Ligi Kuu.

"Timu inapaswa kubadilika kila wakati na kuimarika kwa sababu kiwango sio kizuri sana," alisema.

"Nadhani tuko katika hali nzuri. Nadhani tulicheza mechi zenye ushindani mkubwa. Liverpool ulikiwa mtihani mkubwa sana. Nadhani tulianza mchezo vizuri sana. Baada ya dakika sita au saba tulipaswa kuwa 2-0 mbele. Kisha tukapoteza udhibiti, hasa kwa mambo mawili ambayo hatukufanya vizuri na tukawaruhusu kukimbia katika nafasi, jambo ambalo ni hatari sana dhidi yao.

"Kipindi cha pili tuliimarika sana na tulistahili zaidi. Lakini haikuwa nzuri, kulikuwa na ugumu sana kucheza. Tumepata mengi kutokana na hilo kwa hivyo nimefurahishwa sana.

"Ni wazi tunaweza kuimarika. Mchezo ungekuwa tofauti sana kama nafasi ya kwanza tuliyoipata, tungefunga lakini hilo ndilo goli. Inaleta tofauti unapokuwa kwenye maeneo hayo kwenye eneo la hatari, ukiweka mpira ndani, nyuma ya wavu na tukaunda hali, tulikuwa na nafasi zingine mbili au tatu za wazi ili kuwa bora lakini hatukufanya hivyo, kwa hivyo lazima tujiimarishe."




# IBRAHIMOVIC: SHERIA NYINGI ZINACHELEWESHA UKUAJI MLS

**LOS ANGELES,** Marekani

NYOTA wa zamani wa LA Galaxy, Zlatan Ibrahimovic amesema kwamba Ligi Kuu ya Soka ya Marekani haikui haraka iwezekanavyo kutokana na kuwa na sheria nyingi.

Ibrahimovic, mmoja wa wachezaji waliopambwa zaidi katika miongo miwili iliyopita, alitumia misimu miwili na Galaxy kati ya 2018 na 2019 kabla ya kurejea Ulaya kumalizia soka yake na AC Milan.

Tangu kuondoka kwake, MLS imepanuka kutoka timu 24 hadi 29 huku San Diego FC ikitarajiwa kucheza kwa mara ya kwanza kama timu ya 30 ifikapo mwaka 2025 na kukaribisha rekodi ya mshindi wa Ballon d'Or mara nane Lionel Messi kwa Inter Miami mwaka jana.

Lakini Ibrahimovic, ambaye sasa ni mshauri mkuu wa Milan, aliiambia First Take ya ESPN kwamba anaamini inaweza kuboresha kiwango cha MLS ikilinganishwa na mashindano ya juu barani Ulaya.

"Inakua katika mwelekeo sahihi lakini nadhani inakua polepole kwa sababu nilipokuwa hapa nakumbuka kuna sheria nyingi zinazokwamisha kukua haraka," alisema.

"Lakini linapokuja suala la mchezo, ubora, watu binafsi, mchezo unakua na kuwa bora zaidi. Na kuna Kombe la Dunia pia mwaka 2026 ambalo litakuwa muhimu kwa nchi na MLS."

Nyota huyo wa zamani wa Manchester United, Inter Milan na Paris Saint-Germain pia alisema MLS inahitaji kuendelea kutoa vipaji vya vijana na pia kusajili majina makubwa.

"Nadhani unapowaleta wachezaji hawa wakubwa na wanaonesha ubora wao, unaelewa zaidi jinsi kiwango kilivyo Ulaya. Kiwango ni cha juu zaidi Ulaya, kwa heshima kubwa kwa MLS. Lakini inakua. Unahitaji ijenge kutoka msingi, sio tu juu ya nyota wakubwa wanaokuja na kucheza tu," alisema

## Ten Hag ataka aungwe mkono Man United



**LOS ANGELES,** Marekani

ERIK ten Hag ametoa changamoto kwa wamiliki wapya wa Manchester United "kuthibitisha" kwamba wanamuunga mkono kwa kushikamana naye katika nyakati ngumu msimu ujao.

Ten Hag amedumisha kibarua chake licha ya kumaliza katika nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu msimu uliopita chini ya uongozi mpya wa Sir Jim Ratcliffe na Sir Dave Brailsford.

Mholanzi huyo ameongezewa mkataba kwa mwaka mwingine, lakini kuna hisia miongoni mwa mashabiki wengine msimamo wake unasalia kuwa mbaya, haswa ikiwa United haitaanza msimu vizuri.

Ten Ha alisema Ratcliffe na Brailsford wanaweza tu kuthibitisha kwamba wanamuunga mkono kwa kudumisha imani yao wakati wa matokeo mazuri na mabaya.

"Ninahisi kuwa tunaunda kitu na kwamba, tuko kwenye mashua moja," alisema Ten Hag katika mahojiano ya kina huko Los Angeles juu ya ziara ya klabu hiyo.

"Lakini bila shaka huwa ni jambo lililothibitishwa wakati kesi iko hivi. Ninachotumaini ni kwamba tutaepuka hili."

Ten Hag anaunda timu kuzunguka kiini cha wachezaji wachanga wakiwemo Kobbie Mainoo, Alejandro Garnacho na Rasmus Højlund.

Usajili mkubwa zaidi wa United kufikia sasa msimu huu wa majira ya joto ni mlinzi Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18 na Ten Hag alisema wamiliki watahitaji kuwa na subira.

"Kwa wachezaji wachanga kutakuwa na vipindi vya kupanda na kushuka na tunapaswa kutambua hilo," alisema.

"Kila mtu anapaswa kutambua hili ndani ya klabu hii lakini pia nyinyi vyombo vya habari mnapaswa kutambua hili nje. Ni jambo la kawaida kwamba halitaenda hivi tu kwa vijana, wachezaji wachanga hasa."

Wakati huo huo, Ten Hag pia amefichua kuwa Tyrell Malacia anatarajiwa kuwa nje kwa miezi miwili zaidi. Beki huyo wa kushoto hajacheza kwa zaidi ya mwaka mmoja kwa sababu ya jeraha la goti na aliachwa nje ya kikosi kwenye ziara hiyo.

"Hayuko mbali hivyo, lakini sasa yuko katika hali ya maendeleo," Ten Hag alisema.

## Barcelona yakubaliana na Olmo

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imefikia makubaliano binafsi na kiungo wa RB Leipzig, Dani Olmo huku wakiendelea kufanyia kazi makubaliano ya kumsajili mshindi huyo wa Euro 2024, ripoti imefichua.

Nyota mwenzake wa Hispania, Nico Williams pia analengwa na Barcelona lakini kumekuwa na ripoti nyingi zinazosema winga huyo sasa ameamua kubaki Athletic Club kwa ajili ya msimu ujao.

Huku wakielekeza nguvu zao kwa Olmo, Fabrizio Romano amesema kwamba Barcelona wamefikia makubaliano na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye ana nia kubwa ya kurejea Camp Nou.

Mkataba wa miaka sita sasa umekubaliwa kati ya Olmo na Barcelona, ambao sasa wanafanya kazi kufikia makubaliano na Leipzig juu ya ada ya uhamisho.

Ofa ya hivi punde zaidi ya Barcelona ni pamoja na ada ya uhakika ya euro milioni 55 pamoja na euro milioni 4.

Hata hivyo Sport imeripoti kuwa Leipzig haijafurahishwa na ofa ya Barcelona na huenda ikakataa ombi lao.

Mamba hao wa Ujerumani wanataka fedha nyingi haraka iwezekanavyo, wakati Barcelona wanajaribu kutaka kulipa kwa muda mrefu.

Inasemekana kuwa Barcelona inajaribu kutaka kulipa sehemu kubwa ya ada hiyo hadi msimu wa majira ya joto wa 2025.

Licha ya tofauti kati ya pande hizo mbili, maendeleo zaidi yanatarajiwa katika siku zijazo.

Mkurugenzi wa michezo wa Barcelona, Deco sasa anaangazia dili la Olmo, ingawa bado hajakata tamaa rasmi ya kumuunganisha na nyota mwenzake wa Hispania, Williams.

HABARI MICHEZO

# KAGERE APEWA MWAKA MMOJA NAMUNGO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Namungo imetangaza kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Simba, Meddie Kagere kwa kumpa mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia timu hiyo yenye maskani yake mkoani Lindi.

Kagere amesajiliwa mwaka mmoja baada ya mkataba wake wa mkopo kutoka Singida Black Stars kumalizika.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa mabosi wa klabu hiyo wamempa mwaka mmoja baada ya kuridhishwa na kile alichokifanya msimu uliopita.

"Tumemsajili kwa mkataba wa mwaka mmoja, awali alikuwa kwetu kwa mkopo akitokea Singida Fountain Gate ambayo sasa ni Singida Black Stars, amemaliza mkataba huko, tumejadiliana tumeona anatufaa hivyo tumemsajili, kwa maana hiyo Kagere bado ataendelea kucheza soka Tanzania," kilisema chanzo kutoka Namungo.

Kagere, raia wa Rwanda alikuja nchini na kujiunga na Simba 2018, akitokea Gor Mahia ya Kenya na akawa mfungaji bora kwa misimu miwili mfululizo 2018/19 akimaliza na mabao 23, uliofuata 2019/20 akatwaa tena kiatu cha dhahabu akimaliza na mabao 22.

Aliondoka Simba mwaka 2022 na kujiunga na Singida Fountain Gate, kabla ya msimu uliopita kwenda Namungo kwa mkopo.

Tayari klabu hiyo imeshatangaza kuwaacha wachezaji kadhaa wakiwemo, Derick Mukombozi, Hamad Majimengi na wengeo, huku ikiwaongeza wachezaji kama kina Lenny Kisu, Erick Molongi, Rafael Daudi, Djuma Shaaban, Beno Kakolanya na Ritchi Nkoli.

Wakati huo huo, timu hiyo imeichapa Singida Black Stars katika mechi ya kujipima nguvu kujiandaa na Ligi Kuu. Mchezo huo ulichezwa juzi kwenye uwanja wa Black Rhino, Karatu mkoani Arusha huku mabao ya yote ya Namungo yakifungwa na Hashim Manyanya.



Mchezaji wa mchezo wa tenisi kwa walemavu, Pendo James, akipiga mpira kurudisha kwa mchezaji mwenzake katika mazoezi yanayosimamiwa na Kocha Riziki Salum wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na mashindano ya Kimataifa ya wazi ya Kenya mwezi huu, nchini humo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Tanzania kutupa karata nyingine Olimpiki

**Na Shufaa Lyimo**

MUOGELEAJI wa Tanzania, Sophia Latiff, leo anatarajiwa kuiwakilisha nchi shindano la kuogelea katika michezo ya Olimpiki inayoendelea kwenye jiji la Paris, Ufaransa.

Sophia anatarajiwa kushindana katrika bwawa la mita 50 kwenye mtindo huru 'free style' kwa upande wa wanawake.

Akizungumza na Nipashe jana kutoka nchini humo, Sophia alisema kutokana na mazoezi aliyoyafanya anamatumaini makubwa ya kufanya vizuri.

"Tangu tufike hapa tumekuwa tukiendelea kufanya mazoezi kwa ajili ya kuimarisha miili yetu, vile vile nimezoea hali ya hewa kwani haipo tofauti sana na ya nyumbani," alisema Latiff.

Aidha, alisema licha ya mchezo huo kuwa na upinzani, atapambana na kufuata yale aliyoelekezwa na Kocha wake ili aweze kufanya vizuri.

Sophia amewaomba watanzania wamuombee ili atimize malengo aliyojiwekea ikiwa ni mara yake ya kwanza kushiriki mashindano hayo makubwa.

"Ninaomba Watanzania wenzangu waendelee kuniombea ili hapo kesho (leo) niweze kufanya vizuri kwa kupunguza muda katika shindano langu," alisema Sophia.

Alisema anashukuru viongozi wake kwa namna wanavyomtia moyo tangu alipoanza kujiandaa na mashindano hayo hali inayompa matumaini ya kufanya vizuri.

## Fadlu aita mashabiki kuiona Simba mpya

INATOKA UK. 24

alisema Hussein.

Alisema kwa mbinu ambazo wanapewa na Kocha wao Mkuu pamoja na aina ya wachezaji waliosajiliwa wanaona msimu huu utakuwa bora zaidi kwao.

"Tupo tayari, mashabiki watarajie mchezo mzuri, lakini pia watarajie msimu mzuri wa Ligi Kuu na mashindano ya Kimataifa," alisema Hussen.

Wakati huo huo, Kocha wa APR, Hitimana Thierry alisema amejipanga vizuri kukutana na Simba katika mchezo huo na kudai ni maalum kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao.

Alisema anaifahamu Simba na anajua nimoja ya kubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla, lakiniwamejipanga kuonyesha upinzani kwenye mchezo huo.

"Ni mchezo muhimu kwetu sote, kama mnavyojua tutarejea tena hapa Tanzania kucheza na Azam kwenye michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hiki kitakuwa kipimo kizuri sana kwetu," alisema Thierry.

**Nyota wapya kutambulishwa**

Mbali na mchezo huo, leo Simba itawatambulisha kwa mara ya kwanza nyota wake wapya waliowasajili kwa ajili ya msimu ujao.

Wachezaji wapya wa Simba wanaotarajiwa kutambulishwa ni Jushua Mutale, Steven Mukwala, Jean Charles Ahoa, Debora Fernandes Mavambo, Augustine Okajepha, Valentin Nouma na Karaboue Chamou na golikipa wao mpya Moussa Kamara ambapo wachezaji wapya wazawa watakaotambulishwa ni Abdulrazack Hamza, Valentino Mashaka, Omari Omari, Kelvin Kijili, Awesu Awese na Yusuph Kagoma.

## Mdhamini Ligi Kuu kunogesha ushindani

INATOKA UK. 24

"Leo hii kila mtu ni shahidi wa namna ambavyo tuzo hizi zimeongeza mvuto mbele ya wapenda soka wote hapa nchini kutokana na ushindani mkubwa uliopo miongoni mwa wachezaji wanaotajwa kuwania tuzo hizi wakiwemo kutoka ndani na nje ya nchi.

Alisema imekuwa ni fahari kwao kama wadhamini wakuu kupewa heshima hiyo hali iliyothibitisha thamani ya mrejesho chanya kutoka kwa wadau wa mchezo wa mpira hapa nchini.

"Heshima hii tunayoendelea kuipata kupitia mchezo huu pendwa inatusukuma zaidi kuendelea kuwekeza nguvu zetu zaidi si tu kwenye mchezo huu bali pia michezo mingine ikiwemo riadha, golf na michezo mingine ambayo imekuwa ikitusaidia kusukuma agenda zetu mbalimbali zinazolenga kusaidia jamii hususani kwenye masuala ya afya ya mama na mtoto." Aliongeza.

Alisema msimu ujao tuzo hizo zitakuwa nzuri zaidi ya msimu huu na kunogesha zaidi upinzani uliopo kwenye Ligi Bara.

Michezo
Nipashe Jumamosi Agosti 3, 2024

## Arteta: Arsenal inahitaji kuimarika zaidi

UKURASA 21






Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa (wa pili kushoto) akikabidhi tuzo ya Mchezaji Bora Ligi Kuu msimu uliopita (MVP) kwa mchezaji wa Yanga Aziz Ki (wa pili kulia) jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya tukio la utoaji Tuzo za TFF zilizofanyika juzi usiku jijini Dar es Dar es Salaam. Wanaoshuhudia ni Rais wa TFF, Wallace Karia (Kulia) na Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya NBC, Waziri Barnabas (Kushoto). **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Fadlu aita mashabiki kuiona Simba mpya

●●●Asema amekiandaa kikosi chake kuwafurahisha na kuwaburudisha mashabiki, ajivunia kikosi chake kwa....

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Simba, Fadlu Davids, amewaomba mashabiki kwenda uwanja wa Benjamin Mkapa kukiangalia kikosi kipya cha timu hiyo kikitoa burudani kwa kuscheza soka la kuvutia na lenye kasi baada ya kambi ya wiki tatu nchini Misri.

Simba leo inahitimisha kilele cha tamasha lao la kila mwaka la ,Simba Day' kwa kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya APR ya Rwanda, mchezo huo wa kimataifa wa kirafiki unatarajiwa kuanza saa 1:00 usiku.

Fadlu, alisema mchezo huo ni muendelezo wa maandalizi kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika watakayoshiriki msimu ujao.

Alisema anaamini siku ambazo alikuwa na timu hiyo kwenye kambi yao nchini Misri zimemsaidia kujenga timu imara na yenye ujwiano mzuri.

"Siku ambazo tulikuwa kambini tumeweza kucheza michezo ya kirafiki ambayo kwa kweli imetusaidia sana, kwa saa naweza kusema tupo tayari kuonyesha kile ambacho tunacho," alisema fadlu.

Alisema mchezo huo wa leo dhidi ya APR ni muendelezo wa maandalizi yao ya mwisho mwisho kabla ya kuanza msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Baada ya mchezo wa kesho (leo), tutaanza kujiandaa kwa ajili ya michezo ya Ngao ya Jamii kuelekea kwenye Ligi, mchezo huu utatupa picha ya nini tunatakiwa kuongeza kabla ya mchezo huo wa Ngao ya Jamii," alisema Fadlu.

Aidha, nahodha wa timu hiyo, Mohamed Hussein ,Tshabalala' , alisema maandalizi na kambi waliyokaa nchini Misri itawasaidia kufanya vizuri msimu ujao pamoja na mchezo huo kwani tayari walijipanga kukutana na APR.

"Mazoezi tuliyofanya tulipokuwa Misri ninaamini yatatusaidia kufanya vizuri msimu ujao kwa kurudisha mataji yetu yote,

INAENDELEA UK. 23

# Mdhamini Ligi Kuu kunogesha ushindani

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI klabu ya Yanga ikiibuka kifua mbele kwenye tuzo za wachezaji na makocha waliofanya vizuri msimu uliopita, wadhamini wa Ligi Kuu, Benki ya NBC wameahidi kunogesha zaidi ushindani msimu ujao ikiwa ni pamoja na tuzo hizo.

Katika hafla ya tuzo hizo juzi usiku, Yanga iliibuka kinara kwa kubeba tuzo nyingi kupitia wachezaji wake na Kocha mkuu wa timu hiyo Miguel Gamondi aliyepata tuzo ya kocha bora wa msimu.

Kiungo, Stephanie Aziz Ki, aliibuka kinara baada ya kusomba tuzo nne katika hafla hiyo, tuzo alizozipta ni ile ya Mchezaji Bora wa msimu, Kiungo bora, Mfungaji bora pamoja na tuzo ya kikosi bora cha msimu.

Beki wa kati, Ibrahim Bacca naye alipata tuzo ya beki bora wa msimu uliopita.

Mshambuliaji, Clement Mzize aliongeza idadi yatuzo zilizoenda Yanga baada ya kupatav tuzo ya mfungaji bora wa michuano ya Kombe la Shirikisho huku golikipa wa timu hiyo Djigui Diarra akiibuka kipa bora wa michuano hiyo.

Tuzo ya mchezaji bora wa michuano hiyoilienda kwa kiungo wa Azam FC, Feisal Salum ,Feitoto.

Akizungumzi tuzo hizo, Mkurugenzi wa Fedha wa NBC, Waziri Barnabas aliemuwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi kwenye hafla hiyo, alisema benki hiyo kama mdhamini imejipanga zaidi kuhakikisha udhamini wake kwenye ligi unakuwa chachu muhimu katika kuvisaidia vilabu hivyo kuwa bora zaidi kupitia usajili wa wachezaji wenye viwango vizuri zaidi sambamba na kuboresha mabenchi yao ya ufundi.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >